# *MALKIA WA SHEBA*

Nilikuwa nimechelewa kidogo tu usiku wa leo, tulisongamano kwenye magari wala tusingeweza kuingia. Kwa kawaida mimi huchelewa hata hivyo. Si muda mrefu uliopita nilikuwa nikizungumza kwenye kanisa la United Brethren, nao . . . mhudumu akasimama, na kusema, "Ninataka kumtambulisha kwenu mchelewaji Bw. Branham." [Katika Kiingereza, 'the late' inaweza pia ikawa na maana ya 'marehemu'—Mfa.] Vema, nilizaliwa nimechelewa kidogo, nilichelewa kwa arusi yangu, yapata saa mbili, laiti ningeweza tu kuchelewa kwa mazishi yangu sasa, itakuwa sawa. Ndiyo moja ambayo kwa kweli ninataka kuchelewa.

2 Tuna furaha kuwa hapa katika jiji hili la kupendeza. Tulipokuwa tukizunguka kwa gari usiku wa leo, tukija huku, nilikuwa nikiwazia huko nyuma miaka kadhaa iliyopita, tulipokuwa na mkutano hapa, nami nilikuwa nikiwazia ni wakati mzuri jinsi gani watu hapa walituonyesha, jinsi walivyokuwa wazuri sana, naye Bwana akatubariki.

3 Naye Ndugu Bosworth alikuwa pamoja nasi, amevuka bahari sasa Ng'ambo ya pili. Nilienda kumwona kabla tu hajatuacha. Alikuwa, loo, karibu sana na umri wa miaka mia moja, alikuwa ndio kwanza arudi kutoka Afrika, ambako tulikuwa tukifanya umishenari pamoja. Nikamwambia, wakati alipokuwa . . . Kakimbia mbio nyumbani kwake, na hapo alilala maskini yule mzee wetu, amelala pale akifa, ndipo akainua . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] " . . . wapanda farasi wake." [Sehemu tupu kwenye kanda.] . . . kuliwahi kuwa na mtu yeyote aliyekuwa na heshima . . . [Sehemu tupu kwenye kanda.] . . . alikuwa F. F. Bosworth.

4 Alikuwa mtu mashuhuri wa Mungu, mmoja wa wale wa mwanzoni. Alikuja hapa Texas, naye akakaa katika mji mmoja kwa miaka kumi na kuanzisha . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . makanisa saba, na, kwa uamsho mmoja, haukukoma, usiku, ama, siku zote, na, ama, kwa miaka kumi mfululizo, kila usiku, mahali fulani, akifanya mkutano kwa ajili ya . . . hapa Texas.

5 Mlisikia jinsi alivyoenda? Yapata saa moja kabla hajaondoka kuvuka—kuvuka ile njia, alikuwa amelala kwa muda, ndipo akasimama, akaangalia chumbani, na kusema, "Mama!" Na kwa saa moja kamili, ama labda saa mbili, akapeana mikono na marafiki aliokuwa amewaongoza kwa Kristo, nao walikuwa wameondoka kwa miaka hamsini, wamevuka wakaingia Ng'ambo ya pili. Akarudi na kuweka mikono yake chini, akaikunja namna *hiyo*, akaenda kukutana na Mungu.

6 Kamwe sitasahau maneno yake ya mwisho kwangu, alisema, "Hima, Ndugu Branham, vuka bahari upesi sana, huko ndiko mashamba yako wazi." Kisha akasema . . .

Nikasema, "Ndugu Bosworth, ati wewe si mgonjwa?"

Akasema, "Si mgonjwa hata kidogo," kasema, "wakati wangu unakuja sasa, nimeishi maisha yangu."

Nikasema, "Katika maisha yako yote marefu kwa ajili ya Kristo, ni wakati gani uliokuwa bora kwako kuliko zote, Ndugu Bosworth?"

Akasema, "Sasa hivi."

Nami nikasema, "Je, unatambua, basi, ya kwamba unaondoka?"

7 Akasema, "Naam lakini, Ndugu Branham, yote niliyoishia kwa miaka sitini iliyopita yamekuwa ni kwa ajili ya Kristo, na karibu dakika yoyote Yeye ataingilia mlango ule anipeleke Nyumbani." Hiyo ni kweli.

> Maisha ya watu mashuhuri yote yanatukumbusha
> Nasi tunaweza kuyafanya maisha yetu adhimu,
> Kwa kutengana, tunaacha nyuma yetu,
> Kumbukumbu za kudumu.

8 Ninawazia juu ya ushuhuda wake, tena nawazia juu ya Paul Rader, wakati alipotuacha. Ni wangapi waliopata kumjua Paul Rader? Wengi wenu ninyi watu. Alikuwa mtu mashuhuri wa Mungu, akaenda California. Nilikuwa nikiketi miguuni pake nilipokuwa mvulana mdogo. Naye na Luke kwa namna fulani walishikamana, kama vile mimi na mwanangu, Billy. Basi alipokuwa akifa, Taasisi ya Biblia ya Moody ya Chicago ilikuwa imetuma kundi la waimbaji wanne kuimba, nao kidogo walikuwa wakiimba wimbo wa pole pole, *Karibu Zaidi Na Wewe, Mungu Wangu*.

9 Naye Paul, kama mlimjua, daima alikuwa na ucheshi. Aliandika wimbo huu, wimbo wangu wa mara kwa mara, *Amini Tu*. Na yeye—yeye alikuwa na ucheshi, daima alikuwa akitoa kichekesho, kama Ndugu Bosworth, kwa hiyo walipokuwa wakiimba, *Karibu Zaidi Na Wewe, Mungu Wangu*, aliinuka kitandani, kasema, "Aisee, ni nani anayekufa hapa, mimi au nyinyi?" Kisha kasema a—akasema, "Vuta . . . " kasema, "Fungueni mapazia hayo, mkaniimbie nyimbo motomoto za Injili."

Nao wakaanza kuimba, "Pale msalabani ambapo Mwokozi wangu alifia."

Akasema, "Huo unasikika bora zaidi." Akasema, "Yuko wapi Luke?"

Naye Luke hakutaka kumwona ndugu yake akifa, kwa hiyo alikuwa kwenye chumba kingine. Basi akasema, “Yuko kwenye chumba kingine.”

Kasema, “Mwambieni aje hapa.”

10 Luke, jamaa mkubwa mno, kama nyote mlimjua. Yeye, na Paul, na Billy Sunday, na F. F. Bosworth, na hao wote walikuwa, katika siku zao, walieneza Injili katika siku zao. Kwa hiyo basi, wakati wao... Luke akamwambia Paul, ama Paul akamwambia Luke, hasa, akaushika mkono wake, na kusema, “Liwazie, Paul, ama, Luke, tumetoka mbali pamoja, sivyo?”

Kasema, “Naam, tunaye Luke, ama, Paul.”

Paul akamwambia Luke, “Tumetoka mbali.”

Akasema, “Naam, tumetoka mbali, Ndugu.”

11 Lakini kasema, “Liwazie, katika dakika tano kuanzia sasa nitakuwa nimesimama Mbele za Yesu Kristo, nimevikwa haki Yake,” akaufinya mkono wa ndugu yake, akafa.

Nafikiri ilikuwa ni Balaamu wa kale aliyesema, “Jalia nife kama wao.”

12 Loo, sote tuna furaha kuwa Wakristo, sivyo? Sijui tungekuwaje usiku wa leo isingalikuwa kwa ajili ya Kristo? Tungekuwa na tumaini gani? Tungeweza kutulia wapi? Tungeweza kuweka wapi chochote kama msingi leo, nje ya Kristo?

13 Ee, rafiki mwenye dhambi, wewe katika maskini jumba hili la mikutano usiku wa leo, hebu—hebu nikuonye: Ikimbie ghadhabu ijayo. Kuna Mahali pamoja tu pa Kujificha, nina furaha kwamba Mungu alifanya Mji wa Kimbilio, Kristo Yesu, tunaweza kukimbia ndani, na tuko salama.

14 Hivi majuzi nilikuwa India, Bombay, ambako sisi, Bwana alituruhusu kuhubiria umati mkubwa kuliko wote... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] ...wenyeji elfu moja wanaovaa mablanketi wakivunja sanamu zao ardhini, wakimpokea Kristo kama Mwokozi. Nadhani huko India ilikuwa mara tatu ya hao, bali tusingeweza kuwahesabu. Nami...

15 India hasa ni nchi ya lugha mbili. Mnajua ilikuwa inamilikiwa na Uingereza, kisha hivi majuzi tu ikapata uhuru wake kutokana na kufilisika, bila shaka, halafu basi, walikuwa wamefilisika, nao wakapewa uhuru wao, hasa. Ndipo basi, nikachukua gazeti nami nilikuwa nikisoma kwenye safu ya Kiingereza, nalo likasema, “Nadhani tetemeko la ardhi limekwisha sasa, ndege wote wanarudi.” Nami ningetaka kuchukua muda kidogo tu, kuwasimulia hiyo hadithi.

16 Huko India wao ni maskini sana, ninaamini mahali penye umaskini sana nilipowahi kuwa, maishani mwangu, palikuwa ni India. Ninyi watu hamtambui mpaka iwabidi

kwenda huko wakati mmoja, muwaone maskini akina mama wamelala barabarani, watoto wao wachanga wasio na nyama usoni mwao, maskini matumbo yamevimba, wanakufa kwa njaa, wakiomba chakula. Wanakuomba umchukue huyo mtoto mchanga, umwache yeye afe, bali akijaribu kumwokoa mtoto wake mchanga. Ukimchukua *huyu*, vipi kuhusu *yule*, *huyu*, *yule*, *yule*? Kila mahali tu. Hakika ni jambo la kuhuzunisha, na—nao moyo wangu ulivunjika kuiona India. Natumaini kurudi tena msimu huu wa kupukutika majani.

17 Katika hilo gazeti, lilisema ya kwamba ndege wote walikuwa wameruka wakatoka matunduni mwao. Huko India, hawana nyua nzuri kama mlizo nazo hapa Marekani, waya uliofumwa, na kadhalika, na nyua nzuri za vigingi, kwa kawaida wao huokota mawe, na kuyalundika hayo mawe pamoja. Kuna watu milioni mia nne na sabini nchini India, na kusema kweli, najua ninatia chumvi, lakini ningekisia ombaomba milioni mia nne, wao tu, hawajui chochote ila kuombaomba. Wana rasilimali nyingi sana, bali si mawazo ya kuziendeleza, yote wajuayo ni kuombaomba na dini.

18 Nami nilikaribishwa alasiri hiyo katika hekalu la Wajaini, na dini kumi na saba mbalimbali, na kila moja ilimkana Yesu Kristo, ama, kwamba Yeye ni Mungu. Kwa hiyo mnaweza kuwazia jinsi walivyo. Wanaamini, wengi wao, katika kuzaliwa tena katika mwili mwingine, wao hufagia barabara wanapopitia, wasije wakakanyaga angalau maskini kiroboto, ama sisimizi, kwamba huenda akawa ni mama yao aliyerudi katika hali hiyo, ama kitu fulani. Sasa, kuwahubiria watu kama hao dhabihu ya Damu!

19 Lakini usiku huo wakati Roho Mtakatifu alipokuja jukwaani! Mtu kipofu kabisa alisimama pale, niliona ono alikuwa anaenda kufunguliwa macho yake, Nikasema, "Ninampa changamoto kila mmoja wenu Waislamu, wengine wote, Wajaini, Makalasinga, na Wabudha, na kadhalika, kuja hapa na kumfungua macho mtu huyu." Nikasema, "Mbona kusanyiko kunyamaza hivi?" Nikasema, "Hamwezi kufanya hivyo, wala mimi, bali Mungu wa Mbinguni, aliyemfufua Yesu Kristo katika wafu, ameahidi mambo haya tunayoyaona. Nami sasa hivi nimeona ono," nisingalisema hivyo kama sikuwa nimeona hilo ono, "huyo mtu atafunguliwa macho."

20 Nikasema, "Sasa, kama manabii wa Kiislamu ni wakuu hivi, hebu waje wakamfungue macho, nami nitakuwa Mwislamu." Nikasema, "Mlidhani ilikuwa ni telepathia, ati nilikuwa nikisoma mawazo yake nilipomwambia ya kwamba ilimpasa kuwa na watu watakatifu. . ." Loo, inakubidi tu kwenda kule, angalau, upate kulielewa.

21 Nilisema ya kwamba yeye, "Mtu huyu ni kipofu, alipata upofu kwa kuliangalia jua, yeye ni mwabudu jua. Aliabudu

kiumbe badala ya Muumba, tunajua hilo." Kisha nikasema, "Mngefanya nini kama Makalasinga walitaka kumwongoa awafuate? Ama kama Wajaini walitaka awe wao, na kadhalika, wangefanya nini? Kubadilisha tu njia yake ya kuwaza. Tuna jambo lile lile Marekani, Mungu mmoja tu."

22 Nikasema, "Wamethodisti wote wanataka kuwafanya Wabaptisti wote, Wamethodisti; Wabaptisti wanataka kuwafanya Wapresbiteri wote, Wabaptisti; Mpentekoste anataka kuchukua kitu hicho chote. Kwa hiyo haya basi. Ni kitu gani? Badilisha njia yako ya kuwazia. Lakini hapana budi kuwe na kitu ambacho ni sahihi, na kitu kisicho sahihi."

23 Nikashika Kurani kwa mkono mmoja, Biblia katika huo mwingine, nikasema, "Mojawapo ni cha kweli, na kimoja ni cha uongo. Vyote viwili haviwezi kuwa sawa, maana vinatofautiana sana, kimoja na kingine." Nikasema, "Lakini ikiwa Yesu Kristo, Yeye aliyenionyesha ono kwamba atafunguliwa macho, kama akifunguliwa macho, ni wangapi wenu ninyi watu sasa, kwa kuwa kuhani wenu, ama hakuna mtu mwingine hapa anayeweza kuyafungua macho yake, na mtu anasema atamtumikia Mungu yule atakayemfungua macho, sasa, kama Yesu Kristo atayarejesha macho yake, ni wangapi wenu watakaompokea Yesu Kristo kama Mwokozi wenu?"

24 Kwa umbali tu ningaliweza kuona, hiyo mikono myeusi hewani, ilikadiriwa kuwa watu laki tano. Kwa hiyo, basi mtu huyo alipofunguliwa macho, alinishika kiunoni. Sasa, meya wa Bombay, kweli nilikuwa na jina lake, nikaliweka kwa muda mrefu mfukoni mwangu, alikuwa ameketi pale pale. Na, mbona, walikuwa na wanamgambo, wakavirarua viatu vyangu, mifuko yangu kutoka kwenye koti langu, wangekuwa na watu ishirini ama thelathini, na hao walinzi wakijaribu kuwazuia, nao maskini hao wanawake wangeruka juu ya hao walinzi, wapate tu kukaribia mahali ulipokuwa, wakuguse, wamwache mtoto mchanga akukaribie, ama chochote kile.

25 Wazieni, nao wakiona njaa na kiu kwa ajili ya Mungu namna hiyo, na karibu inakubidi kuwalipa watu Marekani waje kuisikiliza Injili, ama kuhudhuria kanisa Jumatano usiku. Hiyo ni, inasikitisha.

26 Kumalizia hadithi yangu, hao ndege wadogo wanaingia katika haya . . . wanajenga viota vyao katika miamba hii, na pia, mifugo na kondoo huja kutoka makondeni, na kusimama alasiri karibu na vivuli vya kuta hizi, kujikinga na miali yenye joto ya moja kwa moja ya jua hilo la tropiki. Na kwa ghafla hao ndege wakaruka wakaondoka nyumbani mwao wakaenda kondeni, mitini na vichakani, ng'ombe wakaondoka kando ya hizo nyua, kondoo wakaenda kondeni na kusimama wakiegemeana, jambo fulani lilikuwa karibu kutukia.

27 Kwa ghafla, tetemeko la ardhi likatokea na kuzitikisa kuta zote zikaporomoka. Kama maskini hao ndege wangalikaa kwenye viota vyao, wangeuawa, kama ng'ombe na kondoo wangekaa karibu na kuta hizo, wangeuawa. Walikaa huko nje siku mbili, maana, mara kwa mara, matetemeko ya nchi yalikuwa yakija, madogo kwa makubwa. Ndipo baada ya kitambo kidogo, wale ng'ombe na kondoo wakarudi tena, hao ndege wakaruka wakarudi kwenye nyumba zilizokuwa zimesalia kwenye kiota miambani, na kadhalika. Nalo gazeti likasema, "Hiyo ni ishara ya kwamba matetemeko ya nchi yamekwisha."

28 Sasa angalieni, Mungu aliyewaongoza hao ndege, na kondoo, na ng'ombe kuingia ndani ya safina ni Mungu yeye yule anayeweza kuwaongoza leo, Yeye aliwaongoza. Na kama ndege, mnyama, kwa silika, anajua jinsi ya kuiondokea hii minara mikubwa ya Babeli inayokaribia kuporomoka, ni zaidi sana jinsi gani wanaume na wanawake waliozaliwa mara ya pili wanapaswa kujua jinsi ya kutoroka, kuegemeana?

29 Kama kuliwahi kuwa na wakati tunaopaswa kuegemeana, ni sasa hivi. Tuje pamoja, sisi sote pamoja, na tukae pamoja, kwa maana hii minara mikubwa ya mfumo huu mkuu wa ulimwengu, itapita, ili kuingia kwa Ufalme usio na mwisho, ule Utawala wa Miaka Elfu uanze moja ya siku hizi. Juu ya jambo hili, hebu na tuliendee Neno sasa, na kabla ya hapo, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa ajili ya maombi.

30 Sijui, kabla tu hatujaomba, kama kungekuwako na mwanamume ama mwanamke yeyote nje ya Kristo, angetaka kukumbukwa katika maombi haya, waweza kuinua mkono wako? Useme tu, "Nikumbuke, Ndugu Branham." Mungu awabariki, uaminifu wenu. Ajabu! Mungu na asikie. Mungu awabariki. Mikono dazani moja au zaidi. Mungu akubariki, mama, hilo ni zuri. Huko nyuma kabisa, Mungu anaiona mikono yenu, bila shaka, Yeye huiona. Mungu akubariki, bwana.

31 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja tukikaribia kiti Chako cha haki, na kama tungepata haki, kwa urahisi tungefagiliwa tu kutoka kwenye uso wa dunia, bali tunakuja chini ya Damu ya Yesu, kwa kuwa Yeye alisema katika Maneno Yake Mwenyewe, "Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu nitalifanya." Nasi tunakuja katika Jina la Bwana Yesu, hatuombi haki, Bwana, bali tunaomba rehema.

32 Hadithi tu, Baba, katika ule mkato wa magazeti tulio nao pale, kwamba hao ndege wadogo waliruka, wakaondoka. Loo, Mungu yeye yule ambaye angeweza kuwaingiza ndani ya safina, na kabla ya yale maangamizi yaliyotangulia ile gharika ni Mungu yeye yule leo, anaweza kuwavuta ndege Wake na wanyama Wake kuikwepa hatari, hakika, Bwana, unaweza kutuonya tuikimbie ghadhabu ijayo.

33 Kwa maana mataifa wametenda dhambi, na kumwacha Mungu, wameasi mioyoni mwao. Na hivi karibuni tunatambua ya kwamba kutakuwako na mlipuko wa atomiki kote ulimwenguni, ambao utautikisa ulimwengu huu uwe kesho, Umilele wetu. Ndipo asubuhi moja nzuri, Bwana Yesu na Kanisa Lake watarudi duniani.

34 Loo, siku hiyo na ije, Mungu! Hiyo ndiyo mioyo yetu inatamani, wakati wazee watakapokuwa vijana huko milele, hakutakuwako na wazee tena, wala watoto wa siku chache, watakuwa tu katika fahari hiyo kuu ya ujana milele. Tunakushukuru kwa ajili ya kweli hii kuu, Bwana, ingawa inaonekana ni mbali sana kwetu sasa, lakini hata hivyo, huenda isiwe mpaka kesho, mpaka tutakapoiona.

35 Ninaomba, Baba, kwa ajili ya hawa walioinua mikono yao kwa uchaji na ushujaa usiku wa leo, kwamba walitaka kukupokea Wewe kama Mwokozi wao, wanataka kukumbukwa katika maombi. Mungu, hakuna mtu ulimwenguni anayetosha kuwaongoza watu kama hao, ninatambua ya kwamba Roho Wako ndiye anayefanya hivyo. Ulisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba, na wote alionipa Baba watakuja." Baba, ninaomba ya kwamba utawaokoa usiku wa leo.

36 Jalia jambo fulani lisemwe ama lifanywe kwa njia ambayo watakupokea Wewe kama Mwokozi wao, na kujazwa na Roho Wako Mtakatifu, kwa kuwa tunatambua ya kwamba wale waliotiwa muhuri, mapigo yameagizwa yasimkaribie yeyote wa hao walio na Muhuri wa Mungu katika paji la uso wao. Tujalie, Bwana. Waokoe wanaoweza kuokolewa usiku wa leo, wajaze na Roho Mtakatifu wale wanaomngojea, na uwaponye wagonjwa wote na wanaoteseka.

37 Wabariki watakatifu, Bwana, wape ujasiri mpya, jalia wafunge silaha kwa nguvu zaidi. Bariki kila kanisa, kila dhehebu. Mungu, tunaomba ya kwamba mikono Yako ya rehema itawafikia, na uamsho utatokea katika kila kanisa kupitia jamii hii hapa, na kutakuwako na kuja pamoja kama, upepo unaoenda kasi. Tujalie, Baba. Tuma uamsho kwa watu hawa wazuri sana hapa wanaokupenda. Ninaomba ya kwamba utusamehe makosa na dhambi zetu. Sasa, Baba, mfiche mnenaji, usiku wa leo, katika Damu ya Bwana Yesu, kwa kuwa tunaomba, katika Jina Lake. Amina.

38 Katika maandiko ya Injili usiku wa leo, katika Kitabu cha Mathayo Mtakatifu mlango wa 12, na kifungu cha 42, tunataka kuchukua somo hapo kwa ajili ya muktadha mdogo, Bwana akipenda.

39 Asubuhi ya leo tu ilinibidi kwa namna fulani, kile ninachoita, kuzungumza kwa niaba ya Ndugu Moore. Ilimbidi Ndugu Moore kurudi nyumbani, kwa kuwa anamleta mke wake, na hao wengine, huku chini asubuhi, nasi tunamngojea aje.

Ndugu Moore ni mtu mashuhuri wa Mungu, mtu mashuhuri wa Mungu. Nimemjua tangu nilipokuwa tu ninii—ninii, vema, nilipoanza hudumani, miaka kumi na minne iliyopita katika huduma ya uinjilisti. Amekuwa sehemu nyingi ulimwenguni. Nilimpata, hayupo hapa usiku wa leo kwa hiyo naweza kusema jambo hili, Mkristo wa kweli, mwaminifu, mtu halisi wa Mungu, Ndugu Moore, ana kanisa zuri sana huko juu Shreveport. Bwana anambariki.

40 Sasa, katika Mathayo Mtakatifu 12:42:

> Basi *Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa: kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.*

41 Yesu alikuwa akiwakemea watu, na, kwa sababu walikuwa wameuelewa vibaya Ujumbe Wake, nao walikuwa wakijaribu kuufanya jambo ambalo haukuwa. Alikuwa katika miji yao, na alikuwa akifanya miujiza, na kuonyesha ishara Yake ya Masihi kwa watu, kama tulivyozungumzia jana usiku. Nasi tunaona ya kwamba wale waliokusudiwa Uzima waliliona, wale ambao hawakukusudiwa Uzima hawakuliona.

42 Injili huwapofusha wale ambao ha—hawako tayari kuikubali, na itawapa kuona wale walio tayari kuikubali. Basi hivyo ndivyo ilivyokuwa katika siku Zake, wakati Maandiko yalitaja waziwazi mambo hasa aliyofanya, na kusema angelifanya, na jinsi walivyolikosa, ilionyesha ya kwamba iliwabidi kupofushwa.

43 Hebu liwazieni, maskini hao Wayahudi walipofushwa kusudi macho yetu yapate nafasi ya kufunguliwa. Na sasa, Injili ile ile iliyowapofusha Wayahudi inalipofusha kanisa, jambo lile lile lililoahidiwa hasa, nalo linapitia maili milioni moja juu ya vichwa vyao. Nina furaha mnarekodi hilo.

44 Ninajua hiyo ni BWANA ASEMA HIVI ya kwamba I—Injili, Injili ile ile iliyowapofusha Wayahudi sasa inawapofusha Mataifa, kwa sababu ni Injili ile ile, kwa maana hakuna Injili nyingine ila Injili ya Bwana Yesu Kristo. Tuna kanuni nyingi za imani, bali kuna Injili moja. Injili ni nini? Injili ilikuja si katika Neno tu, bali kwa nguvu na madhihirisho, madhihirisho ya Roho Mtakatifu, Mungu akitimiza Neno Lake.

45 Ilibidi iwe hivyo, kwa kuwa katika Marko 16 Yeye alisema, "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuata." Ama vinginevyo, "Enendeni ulimwenguni kote, mkaonyeshe nguvu za ufufuo." Yeye hajafa, bali Yu hai. Naye anategemea mimi na wewe kumruhusu afanye kazi kupitia kwetu kuyafanya mapenzi Yake.

46 Na kama tukipata kukikaribia chochote ambacho si Maandiko, inakubidi kuja kutuambia kukihusu. Hakina budi

kutoka katika Biblia, kupitia Biblia, hakina budi kuambatana na Maandiko mengine yote, na kiwe sahihi. Kama sivyo, basi tu—tuko tayari kusema kwamba ni uongo. Na kama Malaika, ama, kutoka Mbinguni, ama chochote kile, angekuja kuhubiri kitu kingine chochote ambacho hakiko katika Biblia hii, usikisikilize. *Hili* ndilo Neno la Mungu, na Neno la Mungu pekee, nasi tunajua ya kwamba ni kweli.

47 Sasa, tunaona ya kwamba Yesu alikuwa, kabisa, na, amemshawishi kila mwaminio aliyemwamini Yeye, wakati aliposema, "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu, mgeni hawatamfuata." Nasi tuliona jana usiku, katika kutoa kile Mungu alichosema atakuwa atakapokuja, kile nabii alichozungumzia, kwamba Yeye angekuwa Mungu-Nabii. "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi." Nao walijua Masihi angekuwa. . .ishara ya Masihi ingekuwa ni nabii.

48 Hapa wakati fulani uliopita, nikizungumza na rabi fulani, ambapo mtu fulani, John Rhyn, alikuwa kipofu kwa miaka ishirini, akafunguliwa macho, akiombaomba mitaani huko Fort Wayne.

Ndipo rabi huyu akanialika ndani, na kusema, "Uliyafumbua macho ya John kwa mamlaka gani?"

Nikasema, "Kamwe sikuyafungua macho yake."

Kasema, "Vema, ulifanyaje hilo?"

Nikasema, "Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu."

Naye akasema, "Na iwe mbali na Mungu kuwa na Mwana! Roho angewezaje kuwa na Mwana?"

Nikasema, "Rabi," nikasema, "ningetaka kukuuliza jambo fulani: Je, ungeamini manabii? Isingekuwa vigumu kwako kuwaamini manabii?"

Akasema, "Hakika, ninawaamini manabii."

Nikasema, "Isaya alinena habari za nani katika 9:6 aliposema, 'Kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa Mwana?'"

"Vema," akasema, "huyo alikuwa ni Masihi."

Nikasema, "Masihi ana uhusiano gani na Mungu?"

Akasema, "Yeye ni Mungu, Mtiwa Mafuta."

Nikasema, "Niambie mahali pamoja ambapo Yesu aliwahi kushindwa kulitimiza, ila ambapo alionyesha kwamba Yeye alikuwa Masihi Mtiwa mafuta, Bwana Mungu wenu?"

Naye akasema, "Vema, alikuwa ni mwizi."

Nikasema, "Alikuwaje mwizi?"

Kasema, “Aliiba mahindi moja kwa moja kwenye shamba la mahindi.”

49 Nikasema, “Rabi, sheria yenu wenyewe ilisema ya kwamba mtu anaweza kupitia kwenye shamba la mahindi na kula anachotaka, ila hawezi kubeba chochote kwa mfuko.” Hata hakujua hilo, akiwa rabi. Hawezi kwenda zake na chochote, bali iliruhusiwa, Yeye. . . Nikasema, “Hakuiba.” Mwajua, rabi huyo alisimama pale kwa dakika chache. Nami nikasema, “Rabi, hivi huamini kwamba Yeye alikuwa *Huyo*?”

Akasema, “Angalia, bwana,” kasema, “kama ningalihubiri hilo, ningekuwa huko chini mtaani, nikiombaomba.”

50 Nikasema, “Afadhali niwe kule chini nikiombaomba, na kunywa maji ya tawi, kuliko kula kuku mara tatu kwa siku, na jina langu liwe katika dhahabu kwenye hekalu hili hapa, na kujua nilikuwa makosani. Afadhali niwe mkweli.”

Ndipo akaanza kulia, kisha akageuka, akasema, “Nitakuona baadaye.”

Nikasema, “Wewe si mwaminifu kwangu, Rabi.”

Akasema, “Ninaamini kama hao makuhani wa hekalu wangalimsikiliza Yeye, tungekuwa bora zaidi leo.”

Nami nikasema, “Basi wewe amini. Vipi kuhusu hilo?”

Akasema, “Ninaamini Yeye alikuwa ni Mtu mwema.”

Nikasema, “Rabi, unaamini Yeye alikuwa ni Mtu mwema?”

Kasema, “Nitaenda mbali zaidi ya hapo pamoja nawe, ninaamini Yeye alikuwa ni nabii.”

51 Nikasema, “Hayo ndiyo yote ninayotaka useme. Basi alisema Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, halafu basi, kama alikuwa ni nabii, hawezi kusema uongo, kwa hiyo basi, unaamini Yeye alikuwa ni Nabii, Mwana wa Mungu, alionyesha ishara ya Masihi.”

Naye asingezungumza nami tena, akaenda mahali hapo.

52 Loo, ndugu, yale tamaa ya pesa itafanya! Yale upendo wa namna fulani wa kikanisa utakayofanya! Lakini kile upendo wa Mungu utakachofanya basi, kwa moyo ulio tayari kujisalimisha kwa mapenzi na njia za Mungu!

53 Yesu alikuwa amewathibitishia, kasema, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi, bali kama nikizitenda hizo kazi,” kasema, “zisikilizeni kazi basi, kama hamwezi kuniamini Mimi.”

Wakasema, “Yeye, akiwa ni mwanadamu, anajifanya mwenyewe Mungu.”

Kasema, “Kama nikizitenda kazi za Mungu, basi mna nini cha kusema kuzihusu?” vinginevyo.

54 Sasa, tunaona ya kwamba Yeye alifanya mambo hayo, ishara hizo na maajabu mbele zao. Na wengi wao. . .Mataifa hawakuiona kwa sababu hawakujua lolote kuhusu kuja kwa Masihi, bali Wayahudi na Wasamaria waliona ishara hiyo ya Masihi, na mara walipoiona, wakasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli."

55 Yule mwanamke kisimani alisema, "Tunajua ya kwamba Masihi yuaja na atafanya mambo haya, lakini hapana shaka Wewe ni nabii wake."

Yesu alisema, "Mimi Ndiye."

56 Loo, kamwe hapakuwapo na mtu angaliweza kusema hayo ila Yeye, hawezi kuwako tena, kwa sababu Yeye alikuwa Ndiye pekee. Hiyo ni kweli.

57 Sasa, nao wakashindwa kuiona, na wakati walipoiona, walidhihaki na kusema ya kwamba alikuwa akifanya hivyo kwa pepo mchafu, ya kwamba alikuwa ni Beelzebuli. Kwa maneno mengine, Beelzebuli ni ibilisi, kwa maneno mengine, nguvu za ibilisi, Yeye alikuwa mpiga ramli. Nao walidai kuwa ni mpiga ramli kwa sababu Yeye aliweza kutambua mawazo niani mwao, na kuwaambia, "Mbona mnafikiri mioyoni mwenu? Nilikuona ulipokuwa chini ya mti. Jina lako ni Simoni, jina la baba yako ni Yona."

"Mbona," wa—walisema, "yeye ni mpiga ramli."

58 Naye Yesu akasema, "Nitawasamehe kwa kusema hivyo, lakini siku moja Roho Mtakatifu yuaja, na kunena dhidi ya Huyo hakutasamehewa katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao." Kwa hiyo uzito tunaokabiliana nao katika siku hii katika wakati wa mwisho!

59 Tukinena juu ya wakati wa mwisho, ishara aliyopewa Lutu katika siku zake ingeonekana tena katika siku ya mwisho, naye Yesu amesimama pale wakati huo akiitekeleza, nao wakasema. . .Akinena kuhusu siku zilizopita, Naye akaikemea hiyo miji, na kuwaambia juu ya kutokuamini kwao, na ugumu wa mioyo yao, na halafu, hatimaye, akaanza kuzungumza nao juu ya Mungu.

60 Naye Mungu katika nyakati zote na vipindi vyote daima amekuwa na ishara na maajabu miongoni mwa watu Wake. Hakuna kipindi chochote wala wakati wowote, ninataka mwanahistoria yeyote arudi nami hata kwenye *Baraza la Nikea*, ama hata lile *Baraza Lililotangulia Nikea* katika historia, na tuone kama kuna wowote katika, wakati wowote kupitia Luther, Martin, John Smith, Moody, Sankey, Calvin, Knox, Spurgeon, wakati wowote kamwe waliopata kumwagwa halisi kwa uamsho, walikuwa na nguvu za Mungu zilizodhihirishwa miongoni mwao kwa ishara, maajabu, kunena kwa lugha, madhihirisho, uponyaji wa Kiungu, na kadhalika, si wakati mmoja.

61 Na kila walipoanzisha uamsho, mtu fulani aliinuka na kuunda dhehebu nyuma yake, nalo likafa, wala halikurudi tena. Yachunguzeni Maandiko, ichunguzeni historia, mwone kama kila wakati walipowahi kuunda dini ya Kikristo, ilikufa papo hapo, wala haikufufuka tena, haiwezi.

62 Mungu ama ataliongoza Kanisa, au Roho Mtakatifu ataliongoza, ama mwanadamu ataliongoza. Ukimchagua mwanadamu, endelea, Mungu analitoa Kanisa Lake moja kwa moja, Nguzo ya Moto inaendelea mbele, nalo Kanisa linasonga mbele pamoja Nayo.

63 Ana watu binafsi katika kila kanisa, makanisa ya kila namna. Kama mtu ni Mkatoliki, naye anategemea kanisa Katoliki kwa ajili ya wokovu, mtu huyo amepotea, lakini kama yeye ni Mkatoliki, na anamtegemea Yesu Kristo kwa ajili ya wokovu, "Kwa imani umeokolewa, na hiyo ni kwa neema ya Mungu." Kama yeye ni Mbaptisti, Mpentekoste, chochote alicho, ni imani yetu, imani yetu binafsi katika kufa, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu Kristo, Mwokozi wetu.

64 Kamwe usiweke mipaka ya kimadhehebu, tunaamini watu wote wako, wana haki ya kuwa Mkristo, "Yeyote atakaye, na aje." Haidhuru ni rangi gani, kanuni ya imani, kile alicho, kama anamwamini Bwana Yesu Kristo, na amemkubali kama Mwokozi binafsi, ameokolewa kwa imani, hiyo ni neema ya Mungu iliyomwita.

65 Sasa, tunaona ya kwamba katika nyakati zote Mungu daima amekuwa na ishara na maajabu pamoja na watu Wake, kupitia nyakati zote, kila wakati. Nasi tunarudi nyuma, Yesu alikuwa akizirejea wakati alipoona ya kwamba wasingemwamini kama Masihi, Naye akaanza kuzirejea nyakati zilizopita, akasema, "Amin, nawaambia ya kwamba Yona, katika siku za Yona . . . "

Walikuwa wamemwomba Yeye ishara, wakasema, "Utuonyeshe ishara."

66 Mnaona, haidhuru ni mambo mangapi yaliyotukia, hawakuyaona. Hilo ni jambo lile lile leo, mbona, watu huketi moja kwa moja kando ya mwingine namna hiyo, ndipo mmoja anaweza kuona nguvu na utukufu wa Mungu, na huyo mwingine asione chochote. Mbona, kama vile Paulo, ile Nguzo ya Moto, ilikuwa, Yeye angeweza kuiona vizuri, bali wale waliosimama karibu naye wasingeweza kuiona. Wale mamajusi waliiona ile Nyota, hakuna mtu mwingine aliyeiona, ilikuja moja kwa moja juu ya vituo vya uchunguzi wa anga, na kadhalika, kwa sababu hawakuwa wakiitazamia; huna budi kuwa unatazamia kitu fulani. Huna budi kuja na matarajio, ukiongozwa na Roho Mtakatifu, ndipo Mungu atajifunua Mwenyewe kwako.

Sasa, tunaona ya kwamba wao walisema, "Tunataka ishara kutoka kwako."

Naye akasema, “Kizazi kiovu na cha zinaa hutafuta ishara, wala hakuna ishara kitakayopewa, ila ishara ya Yona.”

67 Aisee, huenda nikasimama hapa kwa dakika moja, kabla sijashuka. . . Tutajaribu kutowaweka muda mrefu kupita kiasi, niliwaweka sana jana usiku. Lilikuwa ni jambo la ajabu sana, nilihubiri mahubiri asubuhi ya leo katika dakika ishirini. Wahudumu, hilo ni zuri kweli. Kwa kawaida inanichukua kama saa tatu kumaliza moja. Lakini watu wengine wanaweza kuhubiri na kusema mengi katika, labda, katika dakika kumi na tano kuliko ningeweza katika saa tatu.

68 Mimi ni—mimi ni mkusini, mimi ni mwenda pole, na kamwe siwezi kuliwazia upesi mno, inanibidi kumngojea Yeye aniambie, ndipo ninalisema. Kwa hiyo, kamwe sikwenda kwenye shule zozote wala seminari, kwa hiyo inanibidi tu kumngojea Yeye, niliseme tu Yeye anapolisema, nimfuate tu Yeye. Lakini nina hakika kabisa niko sawa kama nikimngojea. Mnivumilie tu kidogo.

69 Kwa hiyo basi, tunaona ya kwamba siku za Yona. . . Sasa, watu wengi wanamdhihaki Yona, wakisema, “Yeye alikuwa ni Yona.” Mbona, Yona hakuwa jamaa mbaya, Yona alikuwa ni nabii, naye asingeweza kutoka katika mapenzi ya Mungu namna hiyo, yote yalikuwa ni kwa mapenzi ya Mungu. Kamwe hakupanda merikebu mbaya, alipanda merikebu sahihi.

70 Je, uliwahi kusoma historia ya Yona? Ni nzuri sana! Mwajua, sikuzote nilimhurumia chini katika tumbo la yule nyangumi, alifungwa mikono yake, na miguu yake imefungwa, na katika bahari yenye dhoruba, na kutupwa nje, ndipo nyangumi akammeza. Na wakati nyangumi. . . Samaki hula, halafu akiisha kula, anashuka chini na kupumzika huko chini. Hebu walishe maskini samaki wako wa dhahabu kisha uwaangalie, watashuka chini, wayalaze maskini mapezi yao chini, baada ya kulijaza tumbo, na—na—na kupumzika kidogo.

71 Vema, nyangumi huyu alikuwa amemshiba nabii huyu, ndipo akashuka chini ya bahari. Naye alikuwa amelala pale huku mikono yake imefungwa, miguu yake imefungwa, na katika matapiko ya nyangumi, tumboni mwake, labda kina cha mikono ishirini, na chini ya bahari, na bahari yenye dhoruba juu, na amelala pale, kila mahali alipoangalia palikuwa ni tumbo la nyangumi, akaangalia mbele, palikuwa ni tumbo la nyangumi, upande wa nyuma ulikuwa ni tumbo la nyangumi, kila mahali. Ati unanena kuhusu dalili? Alikuwa nazo, mbaya.

72 Lakini mnajua kile ninachopenda kumhusu Yona? Alikataa kuona yoyote ya hizo, akasema, “Kwa mara nyingine tena nitaangalia kuelekea hekalu Lako takatifu. Mambo haya ni ubatili wa uongo. Naangalia kuelekea hekalu Lako takatifu, kwa sababu wakati Sulemani alipoliweka wakfu hekalu aliomba, na kusema, ‘Kama watu Wako wakiwa katika shida wakati

wowote, na watazame mahali hapa patakatifu, basi sikia kutoka Mbinguni.'" Na, mwajua, huko chini katika tumbo la nyangumi huyo Yona angali alikumbuka ya kwamba maombi hayo yalitosha, naye akasema, "Mara nyingine tena nitaangalia kuelekea hekalu Lako takatifu." Naye Mungu akamfanya nyangumi huyo ampeleke mahali Mungu alipomtaka aende hasa.

73 Basi ikiwa Yona chini ya hali hizo, hakuna mtu hapa aliye katika hali mbaya hivyo, hakika hakuna, chini ya hali hizo angeweza kuangalia kuelekea kwenye hekalu lililojengwa kwa mikono ya wanadamu, na maombi ya mtu ambaye alikuwa ni mwanadamu, aliyerudi nyuma baadaye, na angeweza kuamini ya kwamba Mungu alisikia maombi yake, na Mungu akayajibu kwa njia ya kumkomboa chini ya hali kama hiyo, ni zaidi sana vipi sisi, usiku wa leo, tunavyopaswa kuangalia mbali na dalili zetu kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, ambapo Yesu ameketi na nguo Zake Mwenyewe zilizolowa damu, na Mwana wa Ukuu huko Juu kufanya upatanisho?

74 Kataa kuangalia ugonjwa wako. Kataa kuona chochote kinyume na. . .Kuwa kama Ibrahimu wa kale. Alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, Sara alikuwa na sitini na mitano, naye Mungu akamwambia atapata mtoto kwa Sara, akaamini. Miaka ishirini na mitano haikumbadilisha hata kidogo, "Hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini."

75 Ninaweza kumsikia akisema baada ya siku thelathini za kwanza. . .Alikuwa ameishi naye tangu alipokuwa mtoto, ama, msichana, alikuwa ni dada yake wa kambo, naye alikuwa tasa, vivyo hivyo na yeye. Ndipo akasema. . .Naye alikuwa amepita umri wa kuzaa, amepita umri wa kukoma hedhi, mkewe alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano, yeye alikuwa na sabini na mitano. Nami nawazia baada ya siku *kadha* alisema, "Unajisikiaje, Mpenzi?"

"Hakuna tofauti."

76 "Mungu asifiwe, tutampata, kwa vyovyote vile. Nenda katikati ya mji, ukajinunulie lundo la vijiatu vya waridi, na jicho-ndege, na pini. Jiandae, tutampata, kwa vyovyote vile." Mbona walidhani alikuwa mwendawazimu!

77 Nao watafikiri una kichaa, maadamu unamwamini Mungu kwa Neno Lake, na kukana chochote kinyume Chake.

78 Alijua Mungu aliweza kudumisha yale aliyokuwa ametenda, nasi tunapaswa kuwa watoto wa Ibrahimu. Sisi ni watoto wa Ibrahimu iwapo tuna imani ya Ibrahimu. Kila kitu kingine ila Neno la Mungu ni uongo.

79 Angalia yale Mungu aliyosema, tunaangalia yasiyoonekana, unaangalia yale macho yako ya kibinadamu hayaoni. *Huoni* kwa macho yako, kwa vyovyote vile. *Unaangalia* tu kwa macho yako, *unaona* kwa moyo wako. Unaiangalia moja kwa moja, unasema,

"Siioni," unamaanisha huielewi. *Kuona* kwako ndiko ufahamu wako, kwa hiyo unaelewa kwa moyo wako.

80 Sasa, Yona, katika hali hiyo yote, Mungu aliyaheshimu maombi yake. Kuna jambo moja kulihusu, mtoto wa kweli wa Mungu, huwezi kumtenganisha na maombi. Walijaribu kuyatokosa yamtoke Yohana, kisha wakamweka kwenye kisiwa cha Patimo baada ya kumchemsha katika grisi kwa saa ishirini na nne, usingeweza kuyachemsha yamtoke; walijaribu kuyatisha kwa baadhi ya simba, kutoka kwa Danieli, asingetishika; walijaribu kuyateketeza kwa moto pamoja na wana wa Kiebrania, kabisa wakashindwa. Vema, huwezi kumchoma moto umwondoe Roho Mtakatifu, Mwenyewe ni Moto, Moto hupambana na moto. Na wakati mtu kweli amejazwa na Roho wa Mungu, Roho Mtakatifu, huwezi kumchoma moto umwondoe, kumtisha atoke, kumfukuza, atadumu papo hapo.

81 Sasa angalieni, sasa, daima tulifikiri Yona alitoka nje ya mapenzi ya Mungu, hakutoka. Ninawi ilikuwa ni jiji kubwa, lililojaa dhambi, liliorudi nyuma, karibu kama, karibu ukubwa wa St. Louis, jiji kuu, maelfu mengi ya watu mle waliozama dhambini, walikuwa wakiabudu sanamu. Na sasa, sanamu yao kuu, mungu wao mkuu wa bahari, kazi yao ilikuwa ni kuvua samaki, na mungu mkuu wa bahari alikuwa nyangumi, basi wakati nyangumi huyu alipokuja mbio miongoni mwa wavuvi, akautoa ulimi wake kama ubao wa kutembelea, naye nabii akatoka moja kwa moja kwenye kinywa cha huyo nyangumi, hakika, wataamini, Mungu alimleta nabii Wake moja kwa moja kwao. Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo. Huenda likasikika la kijinga, bali hivyo ndivyo alivyofanya.

82 Sasa angalieni, ni njia ya mzunguko kuifikia hoja, lakini angalieni, Yesu alisema, lishikeni hili sasa, hili hapa linakuja, acha moyo wako ufunguke, Yesu alisema, "Kizazi kiovu na cha zinaa chatafuta ishara." Sasa, asingeweza kuwa akiwazungumzia kwa sababu hakuwa amekufa bado, bali alisema watapewa ishara. Ishara: "Kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuwa katika moyo wa nchi siku tatu mchana na usiku." Vinginevyo, kizazi kiovu na cha zinaa kingepata ishara ya namna gani, inayowabidi kupewa?

83 Sasa, unaweza kuzungumza kuhusu ishara zote unazotaka, hii hapa ishara aliyosema Yeye, kwamba kizazi kiovu na cha zinaa . . . Na hii ndiyo! Wasodoma wanaenea duniani, mashaka, kutokuamini, itikadi, mambo ya kila namna yakienea duniani, ni kizazi kiovu na cha zinaa. Lakini Yeye alisema watapokea ishara ya ufufuo. Haleluya! Ati nini? Yesu Kristo akiwa hai miongoni mwetu, akitembea miongoni mwetu, Yeye hajafa, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi," *Mimi* ni kiwakilishi

nafsi, "Nitakuwa pamoja nanyi," si mtu mwingine, "bali *Mimi* nitakuwa, nitakuwa pamoja na . . . "

Nani?

Waaminio. "Ulimwengu hautaniona, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi."

Vipi?

"Ndani yenu."

Umbali gani? Mpaka kizazi cha mitume?

"Hata mwisho wa ulimwengu. Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Mwisho wa ukamilifu.

84 Yule nabii mkuu Eliya kutokea jukwaani, mchukia wanawake, mtu wa nyikani akiwa na Ujumbe wa kuigeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao. Kumbukeni, Yeye alikuwa aje maradufu. Kumbuka katika Malaki 4 (Malaki 3 ilinena juu ya kuja kwa Yohana Mbatizaji, kama Yesu alivyorejea, "Kwa nini nabii alisema, 'Mjumbe wangu?'") lakini kumbukeni, Malaki, huko ni kuja kwa Malaki 4, angalieni kifungu chake cha mwisho, tunajua huyo hakuwa ni Yohana, kwa sababu Yeye alisema ataiteketeza dunia kwa moto, nao wenye haki watatembea juu ya majivu ya waovu. Kwa hiyo halikutukia wakati Yohana alipokuja, bali kwamba Eliya ametabiriwa tena siku hizi.

85 Angalieni, Eliya wa kwanza alikuwa aigeuze mioyo ya baba iwaelekee watoto, Orthodoksi wa kale kwa Ujumbe mpya uliokuwa ukiendelea ambao alikuwa akitoa, na hilo *na* ni kiunganishi cha kukiunganisha kifungu hicho pamoja, "mioyo ya watoto iwaelekee baba zao." Na halafu Ujumbe wa Yohana katika siku za mwisho, ama, Ujumbe wa Eliya, huyo roho atakuwa Kanisani, atakuwa, kuichukua mioyo ya watu waliowaacha baba wa Kipentekoste, na kuigeuza mioyo yao iurudie Ujumbe wa asili wa Pentekoste tena, kama ulivyoanza, yule mjumbe wa agano, ile nyota ya saba ya hiyo siku, tunaishi katika hiyo siku.

86 Angalieni kizazi hiki, kizazi kiovu na cha zinaa, kitatafuta ishara, nao wataipata. Ishara ya namna gani? Ishara ya ufufuo, Yeye hajafa, bali Yu hai. Dini yetu si historia, ni ukweli ulio hai, ni Mungu aliye hai, ni tukio lililo hai. "Kama ilivyokuwa katika siku za Yona."

87 Sasa, Yeye ameendelea, akatoa tamshi lingine, akasema, "Na kama ilivyokuwa katika siku za Sulemani." Huko nyuma katika siku za Sulemani . . . Wakati Mungu anapotuma karama duniani, kama watu wakiipokea, unakuwa ni wakati wa upeo wa ustawi kwao, kama wakiikataa, unakuwa ni machafuko kwao. Angalieni kilichotukia wakati Yesu alipokuwa Ujumbe wa Mungu kwa watu, nao wakaukataa, angalieni kilichowapata watu walioukataa.

88 Katika siku za Sulemani, Sulemani alikuwa ninii . . . utawala wa Sulemani, mhudumu yeyote anajua huo ulikuwa ni wakati wa upeo wa ustawi kwa Israeli, wakati ulio mkuu zaidi. Walijenga hekalu, hawakuwa na vita vyovyote, nao walikuwa pia na nguvu za Mungu miongoni mwao. Loo, karama hiyo ilikuwa kubwa sana, hata mataifa jirani yanawaogopa.

89 Sikiliza, ndugu, kile tunachohitaji leo, hatuhitaji ngome za atomiki, tunachohitaji ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mataifa yataogopa, kama Marekani hii yote inayodai kuwa ya Kikristo itaingia chini ya nguvu za Mungu, kutakuwa na mambo mengi sana yatakayotukia hapa hata kila taifa litaogopa kuachilia bomu la atomiki. Kweli. Yeye ndiye Kimbilio letu, Yeye ndiye Nguvu zetu, Ngao yetu, Kinga yetu, Yote kwa yote kwetu.

90 Sasa, tunaona basi kwamba Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sulemani, Malkia wa Kusini alikuja kutoka pande za mwisho za dunia apate kusikia hekima ya Sulemani." Sasa, katika siku za Sulemani watu wote walikuwa na nia moja, wote waliingia na kuikusanyikia karama. Sulemani alikuwa na karama. Mlijua hilo? Sulemani alikuwa na karama ya utambuzi, naye alikuwa na . . . angeweza kutambua mambo, ikionyesha ya kwamba ilitoka kwa Mungu.

91 Vema, mataifa yote yalikusanyika, na kuingia hekaluni, na kumsikia mtu huyu mashuhuri, Sulemani, wakaangalia hekima yake, na kujua alikuwa ni mwanadamu tu, walijua hiyo ilibidi itoke kwa Mungu. Na, loo, jinsi kila mtu alivyolizungumzia! Kila Mwisraeli angeweza kutokeza kifua chake, aseme, "Hatumtumikii Mungu aliyekufa, tunamtumikia Yule aliye hai. Tunaweza kuwathibitishia, shukeni mje kwenye mkutano usiku wa leo, mwone kama ni kweli ama si kweli." Amina. Ninapenda hilo. Unajua mahali unaposimama basi.

92 "Shuka uje, uone kama ni kweli ama si kweli. Njoo nchini mwetu hapa, uone kama Mungu aliye hai anaweza kuingia ndani ya mtu na kumfanya mtu mkuu mno, karibu hivyo." Amina. Hivyo ndivyo afanyavyo na kila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, mwanamume mkuu mno, mwanamke mkuu mno, mtoto mkuu mno, anaipa kisogo dhambi na mambo ya ulimwengu, na kutembea kwa amani pamoja na Mungu. Ishara kuu, Yeye alisema angetoa ishara kuu.

93 Sasa angalieni, watu wote waliiunga mkono. Si lingekuwa ni jambo zuri sana usiku wa leo kama Marekani yote, sisi sote Wamarekani tungesahau tofauti zetu za kimadhehebu, nasi sote tungeiunga mkono Karama ambayo Mungu alitupa, Roho Mtakatifu? Kila kanisa na kila mtu angeiunga hiyo mkono, mbona, tai- . . . ingekuwa ndiyo gumzo ulimwenguni, kila mahali. Lakini loo, la, "Kama ni dhehebu letu, ni sawa, bali kama dhehebu letu, haiko pamoja nasi, la, ni bure."

Mnaona? Loo, jinsi walivyo wa kimwili! Si ajabu Mungu hawezi kutufanyia lolote. Wakati hali hizo, huna kitu cha kujengea.

94 Angalieni, Yeye kamwe hatajenga juu ya madhehebu yetu, ondoa tu hilo niani mwako. Yeye atajenga juu ya Kristo Yesu pamoja na kila mtu binafsi ambaye atakuja na kumpokea kutoka kwenye dhehebu lolote, moyo wa kweli, mnyofu.

95 Na moja ni kama tu hilo lingine inapofikia hilo, maana yote ni madhehebu, ambayo ni sawa, hilo ni sawa kabisa. Lakini wakati wowote unapoweka . . .

96 Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, "Ndugu Branham, unajua kilichotukia? Dhehebu hili kuu ulilokuwa ukilizungumzia, kasema kwamba daima limekudhamini," kasema, "unajua walichofanya? Walikufukuza, hawatakuwa na uhusiano wowote nawe tena." Kasema, "Waliweka mpaka wao, na kusema, 'Mtu asimpokee Ndugu Branham, tena.'"

97 Nikasema, "Vema, niliweka wangu, pia, nikawapita kwa mbali, na kuwaingiza ndani." Hiyo ni sisi sote, sio mimi, hiyo ni kweli. Ninawaingiza ndani, kwa sababu watoto wengi wa Mungu wako mle ndani, na hiyo ni kweli. Huu Ujumbe ni kwa watoto wa Mungu, si kwa shirika fulani lile, bali kwa watoto wa Mungu. Walinitoa nje, nitawaingiza ndani kwa kutandaza langu kwa upana kidogo, na kuwaingiza tu ndani. Hivyo tu.

98 Kwa hiyo hatuna budi kupendana, kuondoa mashina ya uchungu ndani yetu, ndipo Mungu anaweza kuanza kutenda kazi kupitia sisi, lakini mpaka tutakapopata hilo, basi tu—tuna—tunapigana tu na upepo. Kweli. Hatuna budi kupendana. Yesu alisema, "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa nyinyi ni wanafunzi Wangu." Wema au wabaya, wapende kwa vyovyote vile.

99 Sasa, tunaona basi, ya kwamba—ya kwamba katika siku za Sulemani kila mtu alikuwa na nia moja. Na kila mpitaji, hawakuwa na televisheni wakati huo, Bwana ashukuriwe, bali walikuwa—lakini walikuwa, wao, njia pekee wangeweza kueneza neno ilikuwa ni mdomo kwa sikio. Na kila mpitaji angeingia na kuona mikutano hii mikuu, na kushuka, aiambie nchi yao.

100 Nanyi mwajua, Yesu alisema, "Malkia wa Kusini," ambaye alikuwa wa Sheba, "kutoka pande za mwisho za dunia." Hizo zilikuwa sehemu za mwisho kabisa za dunia iliyojulikana wakati huo. Sasa, kama mtaangalia, ni mwendo mrefu huko chini kupitia Sahara.

101 Sasa, watu wakija na kuondoka, ile misafara ya misafara ya ngamia, na njia ya usafiri waliyokuwa nayo, watu wangeingia, na baada ya kitambo kidogo, misafara ikipitia nchini mwake, maskini Malkia huyu kule chini, labda alikuwa mpagani, kafiri, na kila mtu aliyekuja kutoka huko karibu na Palestina, sikuzote

walikuwa wakisema, "Loo, laiti ungaliona kinachoendelea Palestina. Jamani! Mungu wao ni Mungu aliye hai. Mbona, Yeye amemtia mafuta mtu kule juu, na hata wamemfanya mfalme. Na hekima ya upambanuzi? Hujawahi kuona kitu kama hicho. Isingeweza kuwa ni mwanadamu anayefanya hivyo. Tulimtazama huyo mtu, tukapeana naye mikono, yeye ni mwanadamu, alivaa nguo, yeye ni mwanadamu tu, lakini Mungu amemchagua, na yeye—yeye anafanya mambo ambayo yamepita nguvu za kibinadamu, kwa hiyo tunajua hayana budi kutoka kwa Mungu. Naye anampa Yehova utukufu wote, Mungu wao. Unapaswa kuja, uione!"

102 Loo, mwajua, imani chanzo chake ni kusikia, kusikia habari za Mungu. Vema, maskini moyo wa yule Malkia ukaanza kudunda, "Unajua, ningetaka kuona hilo. Mimi—mimi—mimi . . ." Mwajua, unasikia ushuhuda.

103 Sasa, vipi kama angaligeuza maskini uso wake, uliopakwa rangi, aseme, "*Hmm*! Kama kuna jambo lolote linaloendelea namna hiyo, lingeendelea hapa chini kanisani mwangu, lisingekuwa huko juu"? Vema. Hiyo hadithi isingeandikwa kamwe, Yesu asingemrejelea kamwe, angekuwa ni Yezebeli wa kisasa.

104 Na kwa hiyo, ndipo tunaona ya kwamba maskini mama huyo alianza kuona njaa na kiu. Imani ilikuwa imeshikilia, naye akaanza kumwonea Mungu kiu. Naye Yesu akasema, "Heri wenye njaa na kiu." Hata kuona tu kiu, umebarikiwa kuona tu kiu, kama utapata chochote ama hupati, kuona tu kiu.

Unasema, "Vema, kamwe sijapata chochote."

105 Heri ninyi, kwa vyovyote vile, mnalionea kiu, kwa vyovyote vile. "Heri wenye njaa na kiu ya haki," bali Yeye kamwe hakukuacha umesimama namna hiyo, Alisema, "maana hao watashibishwa." Hilo linanifurahisha sana. "Watashibishwa."

106 Wakati kilindi kinapoanza kuita kilindi, hapana budi pawe na kilindi cha kuitikia wito huo. Kabla hapajakuwapo na kiumbe, hapana budi kuwe na Muumba kuumba kiumbe hicho, ni hayo tu. Njaa na kumwonea Mungu kiu!

107 Ndipo tunaona maskini huyo Malkia amefadhaika sana. Sasa, ni kitu gani kinachotukia kwa kawaida? Sasa, alikuwa na miungu, alikuwa na kanisa, na mchungaji, na labda alikuwa kuhani mpagani, mahali fulani, lakini sasa jambo halisi la kufanya lilikuwa ni kwenda, alipata wazo kwamba alitaka kwenda kuona kama ilikuwa ni kweli. Ninapenda hilo. Ninavutiwa na hilo katika huyo Malkia, namtakia heri, nitamwona katika ufufuo. Naye a—alitaka kujua kama ni kweli au la.

108 Sasa, yeye alikuwa na ujasiri ambao watu wengi hapa, na sehemu zingine za nchi hawana, wanasikia kuhusu kitu kama hicho, "Aa, upuuzi!" Mnaona? Lakini alitaka kujua, kwa hiyo

akasema, “Ninaamini nitapanda niende.” Sasa, ili apande aende, yeye alisema, “Jambo lingine linalonipasa kufanya, sina budi kupata ruhusa kutoka kanisani mwangu,” kama, kwa kawaida, mshiriki mzuri wa kanisa afanyavyo.

109 Kwa hiyo wakashuka kwenda kwa kuhani wake mpagani, naye akasema, “Bwana, baba mtakatifu,” ama chochote alichomwita, na, “Nakwambia kwamba ninasikia habari kwamba kuna uamsho unaoendelea huko Palestina.”

“Loo, nimesikia upuuzi huo tangu nilipokuwa mtoto.” Mnaona?

110 Mwajua, ibilisi humchukua mtu wake, bali kamwe si roho, i—ingali hai. Mungu humchukua Wake, bali kamwe si Roho, pia, Mungu ashukuriwe kwa ajili ya jambo hilo. Roho hufanya vita moja kwa moja kupitia maskani ya mwili hata wakati wa mwisho.

111 “Loo, nimesikia upuuzi hu—huo, huamini hilo. Sasa hebu nikwambie jambo fulani, binti yangu, huna budi kukumbuka, una hadhi kuu, wewe ni—wewe ni mwanachama mwanzilishi wa kanisa letu hapa. Mama yako alikuwa mfuasi wa kanisa hili, nyanya yako alikuwa mfuasi wake, sote huja hapa, mbona, nyanya wa nyanya yako alikuja hapa, wala usingeshikwa na kundi la watakatifu-. . .,” ama, mwajua, “watu kama hao. Usingepanda kwenda kule namna hiyo, ingekuwa ni aibu kwako kushikwa kwenye umati kama huo.”

112 Lakini, unajua, Mungu anapoanza kushughulika na moyo wa mwanadamu, haidhuru wao ni wakubwa jinsi gani, Anawafanya waone jinsi wanavyoweza kuwa duni, mnaona. Akasema, “Lakini, bwana, unajua mimi. . . Kuna kitu *fulani* ndani yangu ambacho ni—ninataka kwenda kuiona.”

113 “Vema, sitakupa ruhusa! Nitalitia mkazo, ninajua wewe ni Malkia, bali mimi ndiye kuhani. Nawe utaleta fedheha juu ya baba yako, na mama yako, na juu ya hekalu hili takatifu, kama ungekutwa na kundi kama hilo. Vema, angalia jinsi walivyo, mbona, wao ni waasi, wao ni bure. Hupaswi kwenda na kujipumbaza na kundi kama hilo. Kama kulikuwa na kitu kama Mungu aliye hai, hebu iangalie miungu tuliyo nayo hapa!”

114 Hiyo ndiyo shida siku hizi, wana miungu wengi kupita kiasi.

115 Kwa hiyo wakasema. . . Akasema, “Lakini angalia, hebu nikwambie jambo fulani, mimi. . . Nyanya yangu alienda hapa, ulisema, babu yangu alienda hapa, na mama yangu alienda hapa, nami nimeenda hapa, nami nimesikia kanuni zenu zote za imani maishani mwangu mwote, walizisikia maishani mwao mwote, wala hatujaona mnong’ono hata mmoja, ama chochote kile, kutoka kwao, imekufa. Lakini wananiambia ya kwamba kuna Mmoja anayeishi huko juu, huyo Ndiye ninayetaka kumjua.

116 "Kama kanuni yenu ya imani ni ya kweli," huenda alisema, "mbona hatuoni kitu kuhusu mungu wenu mnayenena habari zake? Ulisema alikuwako, au kweli alikufa? Alipatwa na nini? Hatujawahi kumwona, Nyanya kamwe hakumwona, na mama yake kamwe hakumwona, na mama yake kamwe hakumwona. Yeye alikuwa Mungu lini?" Ninapenda hilo. Lifanye halisi. "Ni lini alipokuwa?"

117 Mbona, huenda mwanamke huyo, ama, huenda mwanamume alisema hivi: "Sasa, binti yangu, unaelekea kushikwa na . . . kupotoka, hapa, kupata kichaa, utashikwa na ulokole."

118 Lakini akasema, "Bwana, nataka ujue jambo hili: Sijali gharama yake ni nini, na yale usemayo, ninaenda, kwa vyovyote vile." Ninapenda hilo. Si ajabu Yesu alisema atakihukumu kizazi hiki kwenye ufufuo. "Ninaenda, kwa vyovyote vile."

"Tutakutenga! Usirudi hapa te-. . . "

"Kama ni kweli, usijali, sitarudi, kwa vyovyote vile. Sitarudi, loo, la, la! Ninaenda kuona kama ni sahihi kwanza."

119 Ninaweza kumwona sasa, ameliwazia. Sasa, alikuwa na mambo mengi ya kumzuia. Mtu yeyote anayemjia Kristo, usiwe na wasiwasi, ibilisi atakupa mengi ya kukuzuia, hataki ufikie kule, utapitia vizuizi kadhaa kufika kule.

120 Muda si muda mwajua, mbona, ninaweza kuwazia alirudi kupitia ikulu, akaketi chini, akalichunguza. Ninaweza kumsikia akisema, "Sasa, nimesoma Magombo yote ambayo ningeweza kupata juu ya huyo Mungu wao wa kale huko nyuma, huyo, Mungu wa Israeli, Yehova wanayenena habari zake, ninayo Magombo yao hapa katika maktaba yetu, naye kasisi aliyatumia kumkosoa Yeye. Lakini endapo Yehova huyo anamfanyia mwanadamu jambo hilo, hiyo inamaanisha ya kwamba Yehova ni Roho aliye hai aliye ndani ya mtu aliye hai, Yeye anajali kiumbe hai, Yeye si sanamu fulani, ama sanamu fulani ya marumaru, Yeye ni Mtu aliye hai. Kwa hiyo basi tunaenda . . . Nitapanda kwenda kumwona."

121 Sasa, anasema hivi: "Sasa, jambo la kwanza nitakalofanya, nitapanda, kwanza, kupata maoni yangu mwenyewe juu yake. Sitachukua neno la mtu mwingine, kwa kuwa wanakosoa, mmoja akisema *hivi*, na mwingine akisema *vile*. Sasa, hebu niende nikajionee mwenyewe." Ninapenda hilo. Ninapenda hilo.

122 "Hebu niende nikajionee mwenyewe kama ni kweli ama si kweli, hebu nilichunguze. Nita—nitalilinganisha na haya Magombo niliyosoma. Ikiwa Roho aliye juu ya mtu huyo analingana na Magombo yaliyo hapa, nitasema Yehova yuko pamoja naye basi, Naye ni Mungu halisi. Lakini kama tu, Yehova akisema jambo moja wala halitimii, na mambo haya si sawa, basi si zaidi ya sanamu zetu hapa. Kwa hiyo nitapanda huko nikajionee mwenyewe."

123 "Sasa," akasema, "ngoja kidogo, nimekuwa mtoaji mkubwa wa zaka hapa chini, kwa hiyo," sasa, siwapigii debe wahudumu, na kadhalika, lakini yeye alisema, "kama ndivyo—kama ndivyo ilivyo, nitaiunga mkono. Nitachukua dhahabu, na uvumba, na fedha. Kama ni kweli, inastahili kuungwa mkono, kama si kweli, basi nitarudisha pesa zangu."

124 Anapaswa kuja na kuwahubiria Wamarekani wakati fulani, kuunga mkono vitu vinavyokucheka na kukuita mtakatifu anayejibingirisha, na hata hivyo unakiunga mkono. Hiyo ni kweli. Lakini haya basi.

125 Akasema, "Nitajionea mwenyewe, na kama ni kweli, inafaa kila kitu ninachoweza kufanya kuiunga mkono."

126 Na huo ndio ukweli, inastahili . . . si zaidi . . . si asilimia kumi ya pesa zako, inastahili maisha yako yote, inastahili mambo yote ya ulimwengu kwako, kama ni kweli, ni Lulu ile ya thamani kuu.

127 Kama Mungu angali hai, kama Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu aliye hai leo, na yu hai usiku wa leo, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, basi inastahili kila sehemu ya wakati wetu, kipaji chetu, kila kitu chetu, tunapaswa kuuza kila kitu, tuseme kwaheri kwa kila kitu, na kuitumikia. Kama sivyo ilivyo, vema, hima twendeni tu tukajiunge na kitu fulani, na tuendelee, tujiunge na umati mzuri, na kuishi maisha mazuri sana na kuendelea, lakini kama ni kweli, hebu—hebu na tuungane nayo. Kwa hiyo hivyo ndivyo alivyowazia.

128 Basi akawapakia ngamia dhahabu na uvumba, ndipo wazo likaja, mwajua, watoto wa Ishmaeli walikuwa jangwani siku hizo, nao walikuwa ni wanyang'anyi, nao kwa kweli walikuwa wapanda farasi hodari sana, pia, wapanda farasi halisi, wauaji, huko nje jangwani. Naye alikuwa—alikuwa na safari ndefu. Sasa, alianza na maskini wanawali wake na matowashi wake, wachache wao kuvuka jangwa la Sahara.

129 Sasa, ndugu, ninamheshimu mwanamke huyo. Yeye hakuninii . . . Unajua, kuna jambo fulani kulihusu, kama wewe, Mungu kweli ananena na moyo wako, huoni hofu. Kama—kama Mungu alisema na moyo wako na kukwambia Yeye atakuponya usiku wa leo, hujali daktari anasema tatizo lako ni nini, inaondoa tu—inaondoa tu hofu yote ndani yake, kwa namna fulani. Hakujali, alikuwa akipanda kwenda kuona kama ilikuwa ni kweli ama si kweli.

130 Kwa hiyo akaanza kuvuka Jangwa la Sahara. Sasa, angalieni kile maskini mwanamke huyo . . . Labda ilimbidi kusafiri usiku. Hiyo miale ya moja kwa moja ya Jangwa la Sahara! Tena kumbukeni, yeye, inamchukua . . . Mnajua inachukua muda gani kuvuka kule kwa ngamia? Siku tisini, miezi mitatu. Alivuka jangwa hilo, si katika Kadilaki iliyoyoyozwa, gari lililoyoyoyozwa, kama vile watu fulani wanavyoishi hapa karibu na Marekani hii, wasingevuka barabara kuona jambo hilo, bali alivuka hilo

jangwa, siku tisini juu ya ngamia, akiwa na hatari ya kila kitu kilichokuwako, bila kutafuta chochote, lakini maskini moyo wake ulikuwa ukidunda kuona kama Huyo kweli alikuwa ni Mungu aliye hai au la, kwa vyovyote vile. Akashika njia kuiendea.

131 Si ajabu atasimama katika hiki kizazi, katika kizazi hiki na kukihukumu. Alikuja kutoka pande za mwisho za dunia, ulimwengu, chini ya mazingira magumu sana dhidi yake, aje aone kama ilikuwa ni kweli au la.

132 Siku hizi, badala ya kuja kutafuta kujua, watakuja kanisani, labda waketi chini, "Nitaketi kwa dakika moja tu." Baadhi ya wale majirani wema waliwaalika. "Nitaketi, asiposema mambo ninayopenda, nitasimama mara moja nitoke nje."

133 Loo, ewe mnafiki mwenye mashaka! Loo, naam. Simaanishi kukudhuru, lakini ni—ni—ni . . . ni afadhali kukuunguza kidogo kuliko kukuchoma moto. Basi hiyo ni—hiyo ni—hiyo ni kweli. Simaanishi kuwaudhi, simaanishi kufanya hivyo, ninawapenda sana, bali ninajaribu tu kuwaelezea jambo fulani. Mnaona? Loo, jamani! Ni vibaya sana kuishi namna hiyo, ningechukia kuishi namna hiyo.

134 Ndipo basi, huyo hapo anakuja, na sasa, kuvuka hilo jangwa, alikuwa na matatizo hayo yote. Naye alikuwa na siku tisini za kusafiri, labda kusafiri usiku, kwa sababu kulikuwa na joto sana asingeweza kusafiri mchana, na majambazi hao wote, pamoja na pesa hizo zote, na kadhalika. Basi jambo pekee alilofanya lilikuwa na kusudi moja, hilo lilikuwa ni kujua kama kulikuwako na Mungu aliye hai au la, kama Huyo kweli alikuwa ni Mungu aliye hai au la.

135 Kwa nini watu si waaminifu hivyo siku hizi? Kwa nini wasitafute kujua? Yesu huyu ambaye sote tunazungumza habari zake, na tuna kanuni za imani kumhusu, na kanuni za imani za kila namna na kadhalika, hebu: "Je, Yeye yu hai? Yuko wapi? Alipatwa na nini? Biblia ilisema, 'Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.' Yuko wapi?"

136 Anapokuja mjini, mbona—mbona, watu wanaicheka, wanaidhihaki magazeti yanatuma habari mbaya juu yake. Loo, ndugu, si ajabu kuna bomu limetundikwa kwenye mabanda kule kwa ajili yetu! Hiyo ni kweli. Lakini si kwa ajili ya Kanisa, kumbukeni, litakuwa limeondoka, katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho litabadilishwa na kunyakuliwa.

137 Huyo akapitia jangwani, hatimaye, akafika kwenye lango la hekalu. Sasa, kamwe hakuja kuketi tu chini dakika chache, na kusema, "Nitaona sasa, ninaingia, kama hazungumzi kama tu mchungaji wangu, nitachukua tu yangu na kurudi moja kwa moja." Mnaona? La, alikuja kukaa mpaka aliposhawishika,

alikuwa amepiga kambi naye akakaa tu mumo humo nyuani. Ninapenda hilo.

138 "Nitakaa tu hadi mwisho wa uamsho. Nitayachunguza Maandiko yote, nione kama ni kweli ama si kweli. Sitachukua wazo langu la kwanza juu yake, nitaingia tu, nione. Ninajua kile Yehova anachopaswa kuwa, ninajua ahadi Zake ni nini, ninajua Yeye ni Mpambanuzi wa mawazo ya nia, ninajua mambo haya yote, Neno la Mungu ni jepesi, lina ukali, lina nguvu kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, huchoma hata kugawanya mafuta ya mfupa, na ni Mtambuzi."

139 Neno, Neno ni Mungu. "Hapo mwanzo alikuwako Neno. Huyo Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Yeye alikuwa Mungu, nalo Neno, Neno, Kristo, ndani yako, Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo. Loo, enyi kanisa lililolala, amkeni, wahudumu, jitikiseni, saa imewadia, ikimbieni minara hii ya Babeli mwende msalabani, itaporomoka moja ya siku hizi. "Kila mmea ambao Baba Yangu wa Mbinguni hajaupanda utang'olewa. Lakini juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haiwezi kuliporomosha." Hiyo ni kweli. Nina furaha sana.

140 Ufunuo wa kiroho, Kanisa lote limejengwa juu ya ufunuo, "Juu ya mwamba huu." Mprotestanti anasema Yeye alilijenga juu ya Kristo, Wakatoliki walisema lilijengwa juu ya Petro, wote wawili wamekosea, alilijenga juu ya ufunuo wa Petro ya kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Ule ufunuo mkuu, muhimu sikuzote ni kwamba Yesu Kristo ni Nani. Kitabu cha Ufunuo, ambacho ni ufunuo wa Yesu Kristo, kinafunguka na jambo lilo hilo, kuonyesha Uungu mkuu wa Yesu Kristo. "Mimi ndimi Yeye aliyekuwako, na aliyeko, na atakayekuja, Mwenyezi," ufunuo wa kwanza wa funuo zote.

141 Naam, ule ufunuo, "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, Sijali ni mateso mangapi, wanachora mistari mingapi na kukukatilia mbali, nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haitalishinda kamwe." Hiyo ni kweli. Inaonyesha milango yote ya kuzimu ingelipinga, ila isingeweza kushinda. "Nitalijenga Kanisa Langu," Roho Mtakatifu akitenda kazi, akifanya kazi, Kristo aliyefufuka akitenda kazi. Ni nani anayeweza kulizuia? Jaribu. Kamwe hutaweza kufanya hivyo, linaendelea moja kwa moja, tena, na tena. Wainue wakosoaji wote unaotaka, itaimarisha tu Kanisa kila wakati unapofanya hivyo, litaendelea mbele.

142 Kwa hiyo akashuka, akachukua ngamia wake, akarudisha pesa zake kwenye hicho kijisanduku, nadhani, akapiga kambi huko nje. Kwa hiyo, mara ya kwanza kuhudhuria mkutano, alienda asubuhi iliyofuata, nawazia tarumbeta zote zilikuwa zimepigwa, kengele zililia, na nyimbo zikaimbwa, na baada ya kitambo kidogo Mchungaji Sulemani akaja jukwaani.

143 Loo, walikuwa na watu wengi sana pale, labda kadi nyingi za maombi zilisambazwa siku hiyo, nijuavyo mimi, walikuwa na njia fulani. Kwa vyovyote vile, akachukua kiti chake, labda, na kuketi nyuma ya kanisa, hakuna mtu aliyemjua, baraza kubwa asubuhi hiyo. Sulemani akatokea, mtu mzuri sana, akazungumza na watu vizuri sana. Baada ya kufanya maombi na kila kitu, Sulemani akaketi chini. Basi walipofanya hivyo. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Loo, jamani, walikuta kwamba Sulemani alikuwa na namna fulani ya nguvu ndani yake ambazo zisingeweza kuwa ni nguvu za mwanadamu, zilikuwa ni nguvu za Mungu. Akaangalia, kisa kilichofuata, jambo lile lile, kisa kilichofuata, jambo lile lile, kisa kilichofuata, jambo lile lile, kila kimoja hakikukosea.

144 Mimi. . .Nautakia heri maskini moyo wake, ukaanza kudunda, akasema, "Sasa, kama hilo likiendelea, nitajichukulia kadi ya maombi, pia."

145 Kesho yake akahudhuria, hakuwa na haraka, hakuna haraka, alitaka kulichunguza. Akaenda nyumbani, labda usiku kucha akasoma yale Magombo, "Hivyo ndivyo Yehova alivyo hasa, hivyo ndivyo alivyo." Vema. Karudi, "Sijawahi kuona jambo hilo kanisani mwangu maishani mwangu mwote. Haya yote ni mageni kwangu."

146 Anarudi, anaketi chini tena, kesho yake asubuhi, anaiona ikiingia, kisa cha kwanza, kimepambanuliwa kikamilifu, kisa cha pili, kimepambanuliwa kikamilifu, kisa cha tatu, kimepambanuliwa kikamilifu. Jamani, moyo wake ukaanza kudunda haraka zaidi. Hatimaye, akapata njia ya kuingia kwenye mstari wa maombi.

147 Baada ya kitambo kidogo akasimama mbele ya Sulemani. Nayo Biblia ilisema ya kwamba hakuna kitu alichofichwa Sulemani. Haleluya! Akajibu maswali yake yote, hakuna kilichofichika. Kama lilikuwa limefichika kwa mtu mwingine yeyote, halikufichika kwake wakati huo, alimwambia mawazo ya moyo wake hasa. Hakuna kilichofichika, lakini alimjibu yote, roho yake ya upambanuzi ilitambua hasa shida zake zote zilikuwa nini, na kila kitu juu yake.

148 Naye alisema nini? Akageuka, akasema, "Yote niliyosikia ni kweli, na zaidi, hata ni makubwa kuliko nilivyosikia." Naye akasema zaidi ya hayo, "Heri watu walio hapa pamoja nawe kuiangalia hiyo ikifanya kazi kila siku. Heri wale wanaokuja na kwenda pamoja nawe, na kuketi katika kanisa hili, ambao ni washiriki wa hapa pamoja nawe, kuona mambo haya yakitendeka kila siku."

149 Na zaidi ya hayo, akawa Mkristo, akafanya maungamo ya Mungu hadharani. Naye Yesu Kristo mamia ya miaka baadaye alisema, "Atasimama katika Hukumu pamoja na kizazi hiki na kukihukumu kuwa kimekosa, kwa maana alikuja kutoka pande

za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani, na tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani."

150 Nami ninasema usiku wa leo ya kwamba hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani! Bwana Yesu Kristo yupo hapa, aliye mkuu kuliko Sulemani. Mnanisikia? Mkuu zaidi, Yule aliyeahidi, na kusema, "Kazi hizi nizifanyazo, ninyi nanyi mtazifanya."

Itakuwa Nuru wakati wa jioni.
Njia ya Utukufuni hakika mtaipata.

151 Nuru za jioni zinaangaza. Kumbuka, ndugu, jua huchomoza mashariki, hutua magharibi; jua lile lile lichomozalo mashariki hutua magharibi, tunajua hilo. Kijiografia linavuka dunia, namna *hiyo*. Sasa, angalieni kinachotukia. Nabii alisema, "Kutakuwako na siku ambayo isingeweza kuitwa mchana wala usiku." Ingekuwa siku yenye utusitusi, mvua, ukungu, Nuru tu ya kutosha hata ungeweza kuona jinsi ya kujiunga na kanisa, na kuandika jina lako kwenye kitabu, na kuomba msamaha wa Kristo, lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru.

152 Sasa, kumbukeni, ustaarabu umesafiri pamoja na jua. Ustaarabu wa kale kuliko wote ni ustaarabu wa mashariki, Uchina ndio ustaarabu wa kale kuliko wote tunaoujua. Vema. Ustaarabu umesafiri nalo. Sasa, umeenda mbali sana, hata Pwani ya Mashariki na ya Magharibi zimekutana. Tuko kwenye Pwani ya Magharibi, ukienda mbali zaidi, tutarudi mashariki tena, tukiondoka California, tunaenda Japani na Uchina, unarudi tena.

153 Ni kitu gani? "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Tumekuwa na siku, miaka elfu mbili ambapo tumeunda madhehebu, tukajiunga na makanisa, tukajenga vitu vikuu, minara mikuu, hilo ni jema, bali Kristo kamwe hakuagiza hilo. Kamwe hakusema tujenge kanisa, ama kuwa na shu—shule ya theolojia, Kamwe hakuagiza mambo haya, Yeye alisema, "Ihubirini Injili." Tumefanya yale hasa Yeye aliyosema tusifanye. Lakini, kwa vyovyote vile, inapaswa kuwa hivyo. Lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru.

154 Sasa, ingetoa Nuru ya namna gani? Kama hiyo ilikuwa Nuru ya Mwana ya kwanza iliyowaangazia watu wa mashariki, ambayo ni M-w-a-n-a wa Mungu, Naye akafanya mambo aliyofanya kule siku hiyo kwenye Alfa, Yeye hufanya jambo lile lile kwenye Omega. Kama Rubeni na Yaspi; Benyamini, na, ama—ama, Yak-. . ., ama, jiwe la Sardi, Benyamini na Rubeni, wa kwanza na wa mwisho. Sasa, Yeye ni upinde wa mvua katika nyakati zote za kanisa.

155 Sasa, tuko katika wakati wa jioni, Nuru za jioni zimekuja. Na, hakika. . .Ninasema jambo hili, kwa uaminifu wote, Wakristo, nasema hivi, ewe mwenye dhambi, kwa unyofu wote, Mimi—mimi si mhubiri, nadhani, si—sina elimu, bali Mungu alinipa njia nyingine ningeweza kuwaleta watu kwa Mungu,

mnaona, njia nyingine ya, samahani kwa ujinga wangu, kunipa njia ya kuwaombea wagonjwa, roho ya upambanuzi. Sasa, hilo ndilo lililokuwa likihojiwa kule Houston wakati alipojalia picha Yake ipigwe usiku huo, wakati Dk. Best na hao wengine walipokuwa huko nje.

156 Huyo, huyo Malkia aliona nini? Ni kitu gani kilichomfanya atende hivyo? Aliona kitu halisi. Aliona kitu angaliweza kuweka mikono yake juu yake ambacho kilikuwa halisi, si sanamu iliyoketi pale, ambayo mtu fulani alikuwa ameikata kutoka kwenye—kwenye—kwenye marumaru, au kwenye mti, au kwenye udongo, aliona kitu ambacho angeweza kukigusa, ambacho, kitu ambacho kilikuwa halisi. Aliona kitu kilichokuwa hai, kilicholeta Uzima, alijua ilibidi iwe ni Mungu. Aliona kitu... Alikuwa ameona maigizo mengi sana, na udanganyifu mwingi sana, hata akataka kuona kitu halisi, naye Mungu akamruhusu kukiona.

157 Sasa, enyi watoto, leo ulimwengu umejaa udanganyifu, "Njoo ujiunge na dhehebu letu. Kariri kanuni yetu ya imani. Njoo kwenye kanisa letu, lililo kubwa kuliko yote mjini." Ni udanganyifu. Sisemi wao si Wakristo mle ndani. Hiyo si... Lakini kuhusu kanisa kuwa na uhusiano wowote nalo, dhehebu kuwa na uhusiano wowote nalo, hilo ni kosa. Ni udanganyifu tu wa bandia. Kile ulimwengu unachotaka kuona leo ni kitu halisi, halisi, kitu ambacho ni halisi, halisi cha Biblia, halisi cha kiungu.

158 Ninyi nyote mnajua ninawinda, nimewinda maishani mwangu mwote. Mama yangu ni nusu Mhindi wa Cherokee, wala wongofu wangu kamwe haukuniondolea hilo. Kama ninapenda chochote ni hiyo misitu. Loo, ni vigumu kwangu kuvumilia... Ninapoingia kwenye hiyo misitu, ninaanza. Ninamwona Mungu mwituni. Mungu, ninamsikia akiita katika mbweha na mbwa mwitu, namsikia akilia ndani ya kulungu, mbona, hakika. Ninamsikia akipiga makelele katika tai, namwona katika kutua kwa jua, mahali pote ni Mungu. Natoka nje katika maumbile, naiondokea miji hii inayonuka, na kadhalika, ambapo mna dhambi nyingi sana na *uharibifu* unaoendelea wakati wote.

159 Nilisoma gazetini hivi majuzi, ninasahau, ni visa elfu thelathini vya kutoa mimba kwa juma, vinavyofanyika, vilivyorekodiwa katika jiji la Chicago. Je, ni vingapi ambavyo havijarekodiwa? Visa elfu thelathini vya kutoa mimba. Jamani, jamani! Itakuwaje, ndugu? Wazia juu ya ulimwengu mzima, ni kitu gani kinachoendelea wakati huu? Dhambi. Loo, ni mbaya sana!

160 Huko juu katika misitu ya kaskazini, ambako nilikuwa nikiwinda, niliwinda pamoja na jamaa mmoja huko juu aliyeitwa Bert Call, mvulana mzuri sana, mmoja wa wawindaji bora sana niliopata kuwinda nao. Kamwe haikukubidi kumfadhaikia. Haikukubidi...Usingeweza kumpoteza, yeye

alijua mahali alipokuwa. Nasi tulipenda kuwinda sisi kwa sisi, maana tulimwinda kulungu mwenye mkia mweupe.

161 Lakini huyo alikuwa ndiye mtu katili kuliko wote niliyepata kumwona maishani mwangu, alikuwa ndiye mtu mwenye moyo katili kuliko wote niliyepata kumwona. Alikuwa aina nyingine ya nusu chotara, kwa hiyo yeye—yeye . . . lakini mwindaji hodari. Nami nilikuwa napenda kuwinda pamoja naye, lakini alikuwa katili sana, katili sana, alikuwa akiwapiga risasi maskini watoto wa kulungu ili tu kunifanya nijisikie vibaya.

162 Vema sasa, kama sheria inasema unaweza kumpiga risasi mtoto wa kulungu, hilo ni sawa. Ibrahimu alimwua ndama na kumlisha Mungu, kwa hiyo hakuna kosa katika kumwua mtoto wa kulungu kama sheria ilisema ni sawa. Lakini kuwapiga tu risasi kwa furaha ya kufanya hivyo, hilo ni kosa, hayo ni mauaji. Siamini katika kufanya hivyo. Mimi ni mhifadhi, afisa wa uhifadhi kwa miaka mingi, ningali ninaamini hilo, nami ni mwanachama wa mashirika mengi ya uhifadhi. Lakini sasa, hapa ninaliamini, ninaamini—ninaamini katika kuihifadhi.

163 Sasa, na Bert angefanya hivyo tu kwa sababu nilikuwa mhubiri, angenifanya tu nijisikie vibaya. Angesema, "Aa, enyi wahubiri waoga kama kuku," namna hiyo. Alifikiri alikuwa ni jamaa mkubwa, mkali.

164 Kwa hiyo, mwaka mmoja nilipanda kule, naye alikuwa amejitengenezea kijifilimbi. Naye angeweza kulia kama kulungu mdogo, huyo ni mtoto wa kulungu, akimlilia mama yake, naye ange—angepiga filimbi hii ndogo. Kama umewahi kusikia mtoto wa kulungu akilia, ni sauti ndogo, ya kuchekesha.

Ndipo nikasema, "Bert, kweli hutatumia hiyo!"

Akasema, "Aa, endelea, Billy, jirudie."

165 Na vema, tulienda kuwinda siku hiyo, na kulikuwa na yapata inchi sita za theluji, theluji nzuri ya kuwafuatilia, mwishoni mwa msimu. Vema sasa, ni vigumu kuwapata hao kulungu wenye mkia mweupe, mara tu risasi ya kwanza inapofyatuliwa, ndugu, nena kuhusu Houdini, yule bingwa wa kutoroka, yeye alikuwa ni mwanafunzi kwao, wanaweza kutoweka. Wala hawatatoka, inakubidi kuwatoa kwenye hivyo vichaka, uwatikise watoke humo kwa njia fulani, maana watajificha, walale chini, watambae chini ya malundo ya vichaka, kila kitu, watoroke; wawindaji wengi.

166 Hiyo ndiyo sababu ilikubidi kuwa chonjo, kupiga risasi haraka, upesi, kila kitu, kumpata kulungu wako. Basi mimi na Bert tulikuwa tukifanya vizuri sana. Lakini angetaka kuwaua kinyama, angewaua wawili, ama watatu, wanne, watano, chochote alichoweza, ili tu kudhihaki, kumchekelea tu, kisha kunicheka.

167 Siku moja huko juu tulikuwa tumerudi mwituni, ndipo wakati wa chakula cha kutwa ukafika. Sikuzote tulibeba jagi la—la chokoleti moto, kidogo hukutia joto ambapo ukigeuzwa mahali fulani, na ikubidi kukaa nje usiku kucha. Sikuzote tungebeba chakula kidogo cha mchana. Nasi tungewindia kwenye safu ya Rais, Mlima Washington, Adams, juu ya Mlima Cherry, kadhalika, nchi ya kupendeza.

168 Nasi tulikuwa tumeenda huko juu sana kwenye magenge, nyufa, na juu kwa njia hiyo, nasi tulikuwa tumepanda juu sana, na tulikuwa tumewinda hadi yapata saa tano. Tukafika kwenye uwazi mdogo wa ukubwa wa jumba hili la mikutano, naye Bert kwa namna fulani akainama namna *hii*, akaanza kuingiza mkono kifuani mwake. Nikawaza, “Vema, tutaketi, tule chakula chetu cha kutwa.”

169 Kwa kawaida tulitengana, ndipo mmoja akaenda njia moja, na mwingine nyingine, tukirudi nyuma; tukipanda mlimani, tuwinde tukishuka chini, mmoja achukue mteremko mmoja, na huyo mwingine huo mwingine, tukirudi.

170 Na kwa hiyo akaketi chini, nami nikaanza kuketi chini, pia, nami nikaona alikuwa akiingiza mkono mfukoni mwake, kisha akachukua maskini ile filimbi ndogo. Nikawaza. . .Nikasema, “Bert, hutafanya hivyo.”

171 Akacheka tu. Naye a—alikuwa na macho yaliyofanana kabisa na ya mjusi kwangu mimi, kwa namna fulani ni macho yanayofanana na ya mjusi, yako kombo. Akaniangalia, kidogo akitabasamu nusu kwa hayo, yaliyofanana na ya mbwa mwua kondoo, basi akaweka maskini filimbi hii kinywani mwake, naye akapiga tu kama mtoto mdogo wa kulungu anayelia. Basi alipofanya hivyo, kwa mshangao wangu, papo hapo ng’ambo ya uwazi huo kulungu jike mkubwa akasimama.

172 Sasa, kulungu jike ni mama kulungu, kama hungejua. Loo, alikuwa spishi ya kupendeza, masikio makubwa mno, mazuri, macho hayo makubwa ya hudhurungi yakimetameta. Nikamwangalia. Naye akaniangalia kwa macho hayo ya mjusi. Nikasema, “Bert, hutafanya hivyo.”

173 Sasa, hilo—hilo ni ajabu, hawatainuka wakati huo wa mchana namna hiyo. Watakaa. . .Lakini ilikuwa ni kitu gani? Alikuwa ni mama, mtoto mchanga alikuwa akilia. Nami nikamwangalia tena. Ningemwona ameinua kichwa hicho kikubwa akiangalia huku na huku, masikio makubwa yametokeza. Naye akaipuliza tena, ikalia kama mtoto mchanga. Akatokea moja kwa akaingia kwenye huo uwazi. Loo, hilo halikuwa la kawaida sana, hawafanyi hivyo. Nikamwona akitoka huko nje kwenye huo uwazi.

174 Nikawaza, “Uh-loo!” Nami nikamwona akivuta nyuma ule wenzo, akaingiza risasi hiyo kwenye hiyo .30-06. Loo, alikuwa mpiga shabaha hodari. Naye akaweka darubini hiyo chini,

amelenga moja kwa moja moyoni mwake. Nikawaza, "Loo, rehema! Anawezaje kufanya hivyo? Anawezaje kufanya hivyo? Mama huyo wa thamani amesimama hapo akimtafuta mtoto wake mchanga, katika sekunde moja tangu sasa, akagusa kifyatulia risasi hicho kwa risasi hiyo ya mia na themanini ya chembe cha uyoga, angeulipua moyo wake wa thamani moja kwa moja mpaka upande wake wa pili. Nikawaza, "Bert, unawezaje kufanya hivyo? Unawezaje kuwa katili hivyo?" Nami nikamwona na hayo macho ya mjusi, akishuka, nikawaza, "Vema." Nisingeweza kuiangalia, kamwe nisingeweza kufanya hivyo.

175 Naye alikuwa amesimama pale akitembea. Shida ilikuwa ni nini? Yeye hakuwa mnafiki, hakuwa akijaribu kuigiza jambo fulani, alikuwa ni mama, ndani yake alizaliwa kuwa mama. Alikuwa akimtafuta mtoto wake mchanga. Loo, jamani! Alikuwa akimwangalia mtoto huyo mchanga.

176 Baada ya kitambo kidogo, wakati huo mtutu ulipoinuka juu ya kile kichaka, huyo kulungu akaangalia. Sasa, kwa kawaida wataruka, watimue mbio. Vema, upesi *hivyo* wamepotea. [Ndugu Branham alidata vidole vyake—Mh.] Lakini si yeye, alimwona mwindaji, hakutishika, kama tusemavyo, akatazama, akamwona mwindaji, lakini akakifungua kinywa chake mara mbili au tatu, akainua kichwa chake, bila shaka angeweza kutunusa tukiwa tumesimama pale, akaangalia, lakini shida ilikuwa nini? Mtoto wake mchanga, mahali fulani, alikuwa hatarini, silika ya mama.

177 Alijua ilikuwa ni mauti, alijua atakufa, bali hakujali, kulikuwa na kitu ndani yake, upendo wa mama, ukimwongoza kwa mtoto huyo mchanga. "Kwani yuko wapi? Yuko wapi mtoto wangu? Yuko hatarini."

178 Ni—nisingeweza kuangalia tena, kamwe nisingeweza. Nikawazia, "Moyo huo mwaminifu wa mama huyo wa thamani! Bert, unawezaje kufanya hivyo? Wewe ni katili, wewe ni—wewe ni mwovu kufanya jambo kama hilo." Basi nikamwona akiinuka namna *hiyo*, nami nikageuza mgongo wangu.

179 Nikaomba moyoni mwangu, nikasema, "Baba wa Mbinguni, usimwache afanye hivyo. Anawezaje kusimama, akimwona mama huyo wa thamani pale akijaribu kumtafuta mtoto wake mchanga, kisha amdanganye namna hiyo, na kuulipua moyo wake wa thamani, mwaminifu, wa umama kabisa?" Nikasema, "Angewezaje kufanya hivyo, Bwana?"

180 Nikangojea, bunduki haikufyatuka kamwe. Nikangojea kidogo zaidi, haikufyatuka. Nikawaza, "Kwani kuna nini?" Nikaangalia nyuma, nao mtutu wa bunduki ulikuwa ukienda *hivi*.

181 Nikaangalia kote. Akaangalia juu, na machozi makubwa mno yalikuwa yakidondoka machoni mwake, akaitupa bunduki

hiyo chini ukingoni, akasema, "Billy, yamenitosha. Niongoze kwa huyo Yesu unayemjua."

182 Papo hapo kwenye lundo hilo la theluji nikamwongoza mwindaji huyo katili (Ilikuwa ni kitu gani?) kwa Bwana Yesu Kristo. Kwa nini? Aliona kitu halisi, aliona kitu ambacho hakikuwa maigizo, aliona kitu ambacho kilikuwa ni ujuzi halisi wa kuzaliwa, mama.

183 Hivi usingetaka kuwa Mkristo wa namna hiyo? Hivi usingetaka Mungu akufanye Mkristo, Mkristo kadiri mama huyo, kulungu huyo alivyokuwa mama?

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo, na kumwomba afanye hivyo.

184 Baba yetu wa Mbinguni, hadithi ndogo rahisi pale ya—ya Malkia wa Kusini akiona kitu halisi kwa karama ya Mungu. Na hayo makanisa katika New England kule, wao—wao hawakuwa na kitu ila kanisa tu, na kadhalika, mwindaji huyo alikuwa, Wewe unamjua, Bwana, sasa ni ndugu wa thamani, shemasi kanisani, bali kamwe hakuwa ameona kitu chochote halisi.

185 Bwana, Wewe ulisema, "Wakinyamaza, mawe yatapiga kelele." Kitu fulani hakina budi kupaza sauti, "Kuna Mungu aliye hai." Mara ya kwanza mtu huyo alipoona kitu ambacho kilikuwa halisi, alijua kulikuwako na Mungu aliye hai basi. Ulimtumia kulungu kufanya huo mwujiza, na kumleta Kwako mwenye dhambi mwenye moyo katili, kwa sababu mama kulungu alionyesha uhalisi wa umama.

186 Mungu, mfanye kila mwanamume na mwanamke humu ndani, usiku wa leo, Mkristo kama huyo, wanaoweza kuonyesha upendo kama huo mioyoni mwao, kwamba watakuwa ninii, Mkristo mzuri sana, anayeishi maisha yasiyotiwa doa na ulimwengu, mpaka majirani zao watajua ya kwamba wao ni Wakristo halisi, nao wapende kuwa kama wao.

187 Ulisema katika Injili Zako, "Ninyi ni chumvi ya dunia, lakini ikiwa chumvi imepoteza ladha yake." Bwana, hayo ndiyo yanayotendeka kwa madhehebu yetu, yanapoteza ladha yao, wanaweka mipaka, wala hawamruhusu mtu yeyote atoke wala yeyote kuingia. Baba, ninaomba, usiku wa leo, tunajua ya kwamba chumvi ina ladha ikigusa, ninaomba, Mungu, ya kwamba kanisa hili dogo na watu hawa watakolea chumvi sana kwa upendo wa Mungu, hata watawasiliana na kila mwenye dhambi wawezaye, kwa maisha kama hayo, kama hawawezi kuhubiri mahubiri jalia wayaishi, waonyeshe upendo kwa Mungu, kama mama kulungu huyo alivyofanya kwa ajili ya mtoto wake mchanga.

188 Wanangojea, Baba, wapokee katika Ufalme Wako. Wajalie usiku huu, wale walioinua mikono yao, jalia wawe watumishi Wako usiku huu. Naomba uwaonyeshe katika dakika chache zijazo ya kwamba Wewe u hai, hujafa, Wewe u hai milele.

189 Ulisema, "Mimi Ndimi niliyekuwa nimekufa, na ni hai tena, na ni hai milele na milele. Na kwa sababu Mimi ni hai, ninyi pia mtaishi. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Baba, ninaomba ya kwamba utawafanya waaminio, usiku wa leo, kutoka kwa hao wote. Kama hao wako hapa ndani, wasioamini, jalia waende wakiamini.

190 Na sasa ibada iko mikononi Mwako, Bwana, huu ndio umbali niwezao kwenda, ama mtu mwingine yeyote. Lakini tutakapoondoka hapa usiku wa leo, ninaomba ya kwamba watu, wanapoondoka kwenye jumba hili la mikutano, watasema kama wale waliokuwa wakitoka Emau, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu?" Ulitembea pamoja nao siku nzima, hata hivyo hawakukujua Wewe, lakini ulipowaingiza chumbani, halafu ukafanya jambo fulani kama tu ulivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwako, ndipo wakajua ya kwamba Wewe ulikuwa umefufuka katika wafu.

191 Sasa, Bwana, njoo tena usiku wa leo, tumefungiwa humu ndani katika nyumba hii ya wageni usiku wa leo, katika jengo hili dogo la Legion, sasa njoo ufanye jambo usiku wa leo. Onyesha ishara Yako ya Masihi ya kwamba Wewe ni ishara ya Masihi, na hiki ni kizazi kiovu na cha zinaa, na Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele, ya kwamba hii ni kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ulipoketi huku umeelekeza mgongo Wako kwenye hema, na kusema, "Kwa nini Sara akacheka hemani?" na kumwambia Ibrahimu jina la mkewe lilikuwa Sara.

192 Uliahidi ungefanya hivyo, Bwana, tujalie. Ndipo tutakapoondoka hapa usiku wa leo, tutaenda kwenye nyumba zetu mbalimbali tukisema, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo aliposema nasi njiani?" Kwa kuwa tunaomba, katika Jina Lake, na kwa ajili ya utukufu Wake, Jina la Yesu Kristo. Amina.

193 Nitawaombea wagonjwa sasa. (Samahani, Paul.) Nitawaombea wagonjwa. Sina elimu, si—sina nguvu, mimi ni ndugu yenu, natumaini mnaelewa hilo. Nimetumwa kwenu na Mwokozi wenu, na Mwokozi wangu, Mungu wenu, na Mungu wangu.

194 Sasa, wakati mmoja Daudi mchungaji, alikuwa akiwachunga kondoo wa baba yake. Nami nitajaribu kupachukua mahali pa Daudi, sikilizeni kwa makini, nitajaribu kupachukua mahali pa Daudi, usiku wa leo, ninawachunga kondoo wa Baba yangu. Basi siku moja dubu aliingia na kumkamata kondoo, naye Daudi hakuwa mrusha mkuki, wala mtumia panga, kitu pekee alichokuwa nacho kilikuwa ni kombeo dogo, bali alikuwa na neema ya Mungu moyoni mwake,

simba aliingia na kukamata mmoja, alitoka akamfuatilia, akamshika, akamwua, akamrejesha huyo kondoo.

195 Sina dawa, mimi si daktari, nisingeweza kuwa daktari mpasuaji, sijui jinsi ya kutumia kisu, sijui lolote kukihusu, bali kuna jambo moja nililo nalo, hilo ni kombeo dogo la maombi, ni rahisi, lakini siku moja kansa iliingia, na kumnyakua mmoja wa kondoo wa Baba yangu, nikaifuatilia, nikamrudisha huyo kondoo, maombi ya imani yalimwokoa. Ninakufuatilia, usiku wa leo, kwa kombeo la maombi, ninataka kuwarudisha kondoo wa Baba. Niombeeni sasa, tunapoitisha mstari wa maombi.

196 Ninyi Daudi wote humu ndani nisaidieni, kondoo wa Baba ameshikwa na adui, hebu na tumrudishe kwenye afya tena, usiku wa leo. Baba alitwambia tungeweza kufanya hivyo, kama tungeomba lolote katika Jina Lake, Yeye angelifanya, "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usitie shaka, uliyosema yatakuwa yako."

197 Tuliziita kuanzia wapi hizo kadi za maombi? Hivi tulikuwa...? Huh? Moja? Tuliita kuanzia namba moja jana usiku, sivyo? Ati nini? Loo, mlitoa zingine? Zilikuwa zipi? B? Kadi za maombi B. Tuliwapandisha wangapi jana usiku? Kumi na wanane, kumi na wanane? Haichukui wengi.

198 Halafu hao huko nje bila kadi za maombi, hilo ni sawa kabisa, wewe amini kwa moyo wako wote. Mliona jana usiku, kulikuwako na wengi zaidi kwenye kusanyiko, waliokuwa hapa jukwaani.

199 Hebu na tuwaite wachache kutoka kwenye kadi hizo hata hivyo, sasa hivi. Hebu tuanzie, hebu tuseme...Tulikuwa na wangapi jana usiku? Kumi na watano au kumi na wanane? Hebu tuanzie themanini na tano usiku wa leo, kadi ya maombi B, themanini na tano. Ni nani aliye na themanini na tano? Mnaona? Kadi ya maombi B, themanini na tano. Wapi? Loo, samahani. Themanini na tano, njoo upande huu, bwana, yeyote yule. Themanini na sita. Unaweza kuinua mkono wako upesi? Themanini na saba. Hapa. Themanini na saba? Ni nani aliye na themanini na saba? Mama huyu hapa, una themanini na saba? Hapa, mama. Themanini na nane, themanini na tisa. Sikuona themanini na tisa. Waweza kuinua mkono wako? Waangalieni watu kwenye viti vya magurudumu, angalieni mahali walipo. Themanini na tisa. Hebu-...Angalieni...Je, mliiangalia kadi hiyo? Themanini na tisa. Ni nani aliye na kadi ya maombi themanini na tisa? Themanini na tano, themanini na sita, themanini na saba, themanini na nane, themanini na tisa.

200 Sasa, usichukue kadi isipokuwa unakusudia kuja jukwaani, mnaona, ninapoita kuanzia mahali fulani, halafu hakuna anayejibu, basi acha mtu mwingine atakayekuja achukue hiyo kadi. Themanini na tisa, tisini. Ni nani aliye na kadi ya maombi

tisini? Vema. Tisini na moja. Vema. Tisini na mbili, tisini na tatu, tisini na nne, tisini na nne. Sikuiona.

201 Angalieni, mtu fulani hapa, hawa—hawa wanawake wawili walioketi hapa kwenye kiti cha magurudumu, wasingeweza kusimama, kama kadi yao ikiitwa, tutawabeba hapa, mnaona.

202 Tisini na moja, -mbili, -tatu, -nne, -tano. Themanini na tano hadi tisini na tano; tisini na tano hadi mia moja katika kadi ya maombi B. Mwaweza kuja? Tisini. Themanini—themanini na tano hadi mia moja, wale walio na kadi hizo. Ninyi wengine shikilieni tu kadi zenu, tuta—tutazifikia, baadaye. Themanini na tano, themanini na sita, themanini na saba, themanini na nane, themanini na tisa, tisini, tisini na moja, -mbili, -tatu, -nne, -tano, -sita, -saba, -nane, -tisa, mia moja.

203 Sasa, wakati wakiwakusanya hao wachache tutakaoanza nao hapa, huenda tusimfikie mmoja ama wawili wao Sijui, inategemea kile Roho Mtakatifu asemacho, ni wangapi kwenye kusanyiko hapa ambao hawana kadi ya maombi, na hata hivyo unataka, wewe ni mgonjwa, na unataka Mungu akuponye? Inua mkono wako. Vema. Sasa, sikujui. Lakini laiti ungaliangalia tu huku na kuamini! Ni wangapi hawajakuwa katika mmoja wa mikutano yangu hapo kabla? Hebu tuone mikono yenu. Bwana awabariki, tuna furaha kuwa pamoja nanyi usiku wa leo.

204 Sasa, kumbukeni, sidai kuwa mponyaji, ninaamini kuna Mponyaji mmoja tu, huyo ni Mungu. Nami ninaamini ya kwamba tayari amekufanyia kila kitu awezacho kufanya, ni wakati wako basi kukubali yale aliyokufanyia. Lakini kama alikuwa amesimama hapa usiku wa leo, amevaa suti hii, asingeweza kukufanyia zaidi ya yale anayofanya, yale angefanya papa hapa sasa. Hiyo ni kweli?

205 Sasa, katika Biblia. . .Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yesu ni Kuhani Mkuu? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Biblia ilisema ya kwamba Yeye, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu, aliyesimama mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu, akituombea? Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Waebrania 13:8 ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele"? Vema, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule ambaye Yeye alikuwa jana, na Kuhani Mkuu huyu aliyeketi huko Juu, Yeye ni Kuhani Mkuu sasa, aliyeketi huko Juu, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Ni wangapi wanaojua Biblia inasema hivyo, ya kwamba Yeye anaweza kuguswa?

206 Sasa, utamgusaje kama Yeye ameketi huko Juu? Vile vile yule mwanamke alivyomgusa huko nyuma. Haikuwa ni kidole chake kwenye vazi Lake, Yeye hakuhisi hilo, bali ilikuwa ni imani yake. Wengi walikuwa wakimgusa namna *hii*. Lakini Yeye alisema, "Imani yako imekuokoa." Sasa, alimgusa, Naye akageuka wala hakujua ni nani aliyemgusa. Hiyo ni kweli? Akaangalia pande zote, akasema, "Ni nani aliyenigusa?"

207 Ndipo Petro akamkasirikia sana, na kusema, "Vema, Bwana," akamkemea, akasema vinginevyo, akasema, "unazungumzia nini, kwa vyovyote vile? Kwa nini useme jambo kama hilo? Kila mtu anakupigapiga mgongoni."

Akasema, "Naam," kasema, "huu ni mguso wa namna nyingine, ni—nilijisikia Mwenyewe nikiwa dhaifu." Nguvu, huo ni uweza, zilimtoka.

208 Akaangalia kote kwenye kusanyiko, ndipo akamwona maskini mwanamke huyo huko nje, na kumwambia alikuwa akitokwa na damu, na imani yake ilikuwa imemwokoa. Hiyo ni kweli? Sasa, Yeye kamwe hakusema alifanya hivyo, alisema imani yake *Kwake* ilimponya.

209 Vema, sasa, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule usiku wa leo, kama vile alivyokuwa wakati alipokuwa hapa duniani, Naye, Biblia inasema ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, ukimgusa, hivi Yeye hatatenda kama alivyotenda wakati huo? Asingeweza kutenda tofauti, na awe Kuhani Mkuu yeye yule. Ni wangapi wanaojua hilo kuwa ni kweli?

210 Vema, basi wewe, kwa imani, angalia juu, na useme, "Bwana Yesu, Wewe ni Kuhani wangu Mkuu, jalia nikuguse, Bwana, kwa udhaifu wangu, unirehemu. Jalia Ndugu Branham aite sasa, ninajua Yeye ni mwanadamu tu, bali Wewe ungali ni Kuhani Mkuu, na sasa, ninataka kukugusa Wewe, Nawe unene kupitia kwake, na kuniita kama tu ulivyofanya—ulivyomfanyia yule mwanamke." Hilo litaondoa mashaka yote moyoni mwako, sivyo?

211 Loo, hili si ni zuri sana? Si Mungu fulani wa kale, wa kihistoria, bali Mungu sasa hivi.

212 Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yesu Kristo alisema Mwenyewe kwamba Yeye hakufanya lolote mpaka Mungu alipomwonyesha ono kwanza la kufanya? Yohana Mtakatifu 5:19, "Amin, amin, nawaambia," neno "amin" linamaanisha *kabisa*, "Nawaambia, Mwana," hiyo ni kusema mwili Wake, mwili, "hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile." Hiyo ni kweli? Basi hakufanya mwujiza hata mmoja mpaka alipoona ono lake likifanywa. Hiyo ni kweli? Kama hakufanya hivyo, alisema uongo, wala asingeweza kusema uongo, maana Yeye alikuwa ni Mungu. Mnaona? Kwa hiyo ilibidi iwe.

213 Sasa, ninawatakeni mtulie tu iwezekanavyo, na mwe na kicho kabisa, mkeshe, mwombe. Sasa, wakati mwingine wakati upako huu unaposhuka. . . Sisemi kwamba utashuka, usiposhuka, basi jambo pekee ninaloweza kufanya ni kujitolea kwa Mungu, niondoke jukwaani, hivyo tu ndivyo ninavyoweza kufanya. Lakini kama Yeye akija, na kufanya jambo lile lile hapa, na kuthibitisha ya kwamba Yeye angali ni Masihi kwa

Mataifa katika kumalizia kwa wakati wetu kama alivyokuwa kwa Myahudi na Msamaria, je, ninyi watu mtakuja na kumpokea kama Mwokozi na Mponyaji? Mtafanya hivyo, mliamini?

214 Sasa, nijuavyo mimi, katika kusanyiko hili lote sioni mtu mmoja ninayemjua. Jukwaani, kufikia sasa hivi . . . Nilifahamiana na maskini mhudumu huyu tangu nimekuwa hapa, maskini ndugu yetu hapa, mwanangu na wavulana wangu wa kurekodi kanda hapa ndio tu ni—niwajuao.

215 Ninaamini ninamjua ndugu huyu, siwezi kumkumbuka, ninaamini unatoka huko Louisiana, mahali fulani. Hivi sikuenda kuwinda bata wakati mmoja pamoja nanyi, ama nilishuka huko chini kwenu, ama chochote kile? Nikafanya mkutano huko chini kwenye . . . Jina la mahali hapo liliitwaje? DeQuincy. Bennett. Jamani! Samahani, sina budi tu kukupa mkono. Mungu akubariki. Sijakuona kwa muda mrefu. Vema, hujabadilika, nimezeeka. Mnaona, ilinibidi kufanya kazi, labda. [Ndugu Bennett anasema, "Tunataka urudi."—Mh.] Asante, Ndugu Bennett. Vizuri sana!

Katika mstari wa maombi, hivi mimi ni mgeni kwenu nyote? Siwajui? Kama ndivyo, inueni mikono yenu kama mimi—kama hatufahamiani. Vema.

Wote huko nje ambao hatufahamiani, nawe unajua sikujui, inua mkono wako. Mnaona?

216 Sasa sisi hapa. Je, Yeye angali ni Yesu, ama sivyo alivyo? Kama akifanya hivyo, kama atatimiza Neno Lake, Yeye angali ni Mungu. Kama hilo halifai kitu basi, kama Biblia hii hapa . . . Kama Mungu hatatimiza ahadi Yake, basi Yeye si Mungu; kama Yeye kweli hutimiza ahadi Yake, Yeye ni Mungu.

217 Na sasa, wakati alipokuwa hapa duniani, mnakumbuka yale aliyofanya, aliwaonyesha ishara Yake ya Masihi. Nanyi nyote wasomaji wa Biblia mnajua jambo hili, ya kwamba ishara ya Masihi ilikuwa ndiyo ishara ya nabii. Wote wanaojua hilo, inueni mkono wenu, enyi wasomaji wa Biblia. Hakika. "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama mimi."

218 Lakini hao Wayahudi wasingeweza kujibu, kwa hiyo wakasema, "Yeye hufanya hivyo, yeye ni m—mpiga ramli, Beelzebuli, telepathia ya kiakili, ama kitu fulani." Nao wanafanya jambo lile lile leo, bali hilo halimzuii Mungu, anaendelea vivyo hivyo, anaenda tu mbele vivyo hivyo, mtu fulani ataamini.

219 Sasa, kama ningeweza kumponya yeyote kati yenu ninyi watu hapa, ningefanya hivyo, bali siwezi kufanya hivyo. Yesu asingeweza kufanya hivyo, kama angekuwa amesimama papa hapa, nawe ukamjia, angalikuwa amesimama hapa amevaa suti hii aliyonipa Yeye, ungesema, "Bwana, mimi ni mgonjwa, nataka uniponye."

220 Ninawazia Yeye angesema kitu kama hiki: “Mtoto Wangu, hivi huamini ya kwamba nilifanya hivyo? Je, sikujeruhiwa kwa makosa yako, nikachubuliwa kwa maovu yako? Kwa kupigwa Kwangu *uliponywa*. Hivi huamini hilo? Tayari nimekuponya.”

221 Vema, sasa, Yeye alisema nini huko nyuma? “Ninaweza, kama ukiamini.” Vema, tayari imefanywa sasa, kwa hiyo inakubidi tu kuamini, hivyo tu. Kwa hiyo jambo pekee angaliweza kufanya lingekuwa ni jambo la kukuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi.

222 Kwa hiyo, mwili Wake usiku wa leo umeketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu. Tunaamini hilo, sivyo? Siku moja Yeye atarudi duniani katika ule Utawala wa Miaka Elfu, na kuketi kwenye kiti cha enzi cha Daudi. Hiyo ni kweli. Lakini Yeye ameketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu usiku wa leo Utukufuni, akiishi daima kufanya maombezi. Lakini Roho Wake amerudi humu Kanisani, na Roho Wake anafanya jambo lile lile, kama nilivyosema asubuhi ya leo, kama tawi la kwanza la Mzabibu lilizaa kanisa la Kipentekoste, kila tawi halisi kutoka kwenye Mzabibu huo litazaa kanisa lingine la Kipentekoste. Lakini tuna matawi mengi sana yaliyopandikizwa, nayo yanazaa kwa jinsi yake. Tuna tawi la Kimethodisti lililopandikizwa ndani yake, tawi la Kibaptisti, tawi la Kipentekoste, kila aina nyingine ya tawi, linazaa tunda lake lenyewe.

223 Unaweza kuchukua m—mchungwa na kupandikiza mbalungi ndani yake, utaishi kwa uhai wa mti huo, bali utazaa balungi; hebu pandikiza limau mle ndani, litazaa limau, sio chungwa, hata hivyo linaishi kwa uhai wa mchungwa, mnaona, tunda lolote la jamii ya mchungwa.

224 Kanisa lolote linalokiri kuwa la Kikristo linastawi kutokana na utukufu na sifa za Kristo, bali haliwezi kuzaa lile tunda. Halitazaa Uhai wa Kristo mpaka Kristo atakapolizaa tawi hilo Mwenyewe, ndipo litaninii. . . wataandika Kitabu kingine cha Matendo nyuma yake, hiyo ni kweli, kwa sababu ni matendo ya Roho Mtakatifu Kanisani. Mnaona? Hivyo ndivyo ilivyo usiku wa leo, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

225 Na tuombe sasa, kila mtu atulie kabisa, msisogee, tulieni kanisani mwenu, ama vitini mwenu, kitini, popote pale, tulieni tu kwa muda kidogo, muwe na kicho.

226 Baba, hili ni tamshi kuu, lakini hapa usiku wa leo zaidi ya watu mia moja na wachache hapa, walioketi hapa, nimekuomba Wewe ujitokeze, kama kuna makumi ya maelfu, naam, mamia ya maelfu, Wewe hujatupungukia kamwe bado.

227 Siku zangu zinafifia sasa, Bwana, mimi, siku moja itanibidi kuifunga Biblia hii kwa mara Yake ya mwisho. Kama ningeondoka usiku wa leo, Wewe umethibitisha huo ushuhuda kwamba ni wa kweli. Tangu nilipokuwa mvulana mdogo niliwaambia ya kwamba nilikuwa nimeona Nuru, ilikuwa ni ya

kaharabu, kama nguzo. Umeiruhusu sayansi kote ulimwenguni kupiga picha hiyo na kuichunguza, mara nyingi Wewe umekuja, na sasa iko katika *Kodakromu* ya rangi, ulijalia ipigwe majuma machache yaliyopita. Ujerumani, Uswisi, kote ulimwenguni, kamera za taifa. Kama nikifa, kamera ya kimitambo inasema kwamba nimesema kweli, Uwepo Wako wenyewe unaonyesha ya kwamba ilikuwa ni kweli, Biblia Yako inadai kwamba ni kweli. Baba, jalia watu waliamini kwamba ni kweli, na kukupokea Wewe usiku wa leo kama Mponya wao, kama Mwokozi wao, kama Mfalme wao, kama Bwana wao, Ubwana wa kutawala, kuyatawala maisha yao. Tujalie, Bwana.

228 Sasa pamoja na mimi mwenyewe, na kanisa hili, ninayakabidhi yote mikononi Mwako, kwamba huenda ukafanya jambo fulani usiku wa leo, kuwaonyesha watu hawa ya kwamba Wewe ungali ni Mungu-Nabii. Wewe ungali ni Mungu. Unaninii tu. . . Wao. . . Ulikufa ili kuondoa dhambi, bali ulifufuka siku ya tatu. Wewe ulisema, "*Mimi* ninao uweza wa kuutoa uhai *Wangu*, na *Mimi* ninao uweza wa kuutwaa." Hakuna mtu aliyeutoa Kwako, wala hakuna mtu aliyeutwaa. Ulijilaza chini Wewe Mwenyewe, ukafufuka Wewe Mwenyewe.

229 Biblia ilisema Mungu alimfufua, na ni kweli. Baba, Wewe u hai milele, ukiishi mioyoni mwa watu Wako, pamoja na ahadi, "Kazi nizifanyazo Mimi, wao nao watazifanya." Ninanukuu hili, Bwana, kwa sababu Wewe ni mwaminifu kwa Neno Lako, Nawe ulisema kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, itakuwa hivyo wakati tu wa kuja kwa Mwana wa Adamu.

230 Nasi tunakumbuka, wakati ishara hizo zilipofanywa huko Sodoma, ilikuwa ni muda mfupi tu mpaka ule Moto uliposhuka na kuiteketeza Sodoma. Tunautazamia wakati wowote, Bwana. Tunaona ishara ikitokea. Tunaona ulimwengu katika hali ya Sodoma, ahadi za Mungu zikidhihirishwa. Je, utafanya hivyo mara nyingine tena usiku wa leo, Bwana, kwa heshima na utukufu Wake Yeye aliyelifundisha Neno? Ninaomba, katika Jina la Yesu Kristo, kwa utukufu wa Mungu. Amina.

231 Sasa, haidhuru ni nini kinachoendelea, iweni na kicho. Simaanishi ya kwamba hamwezi kumsifu Mungu, bali mumwendee Mungu kwa utulivu, kwa akili timamu, kiajabu, halafu basi, mnapomwona Mungu akifanya jambo fulani, hakika, Yeye anawataka mumwabudu Yeye, ila mje kwa kicho.

232 Sasa, ninyi watu mnapokuja mstarini, mkija hapa, ama huko nje, iweni macho. Ninaangalia, sina mamlaka juu Yake, siidhibiti, inanidhibiti. Ninaweza tu kunena yale inayoniambia, ninaweza tu kunena, na mahali ilipo, ninaiangalia, popote ilipo, hapo ninaiangalia, na kuona kile inachofanya.

233 Sasa, jana usiku mtu wa kwanza tuliyekuwa naye jukwaani, ninaamini alikuwa ni mwanamke. Hiyo ni kweli? Huyu ndiye huyo mtu? Vema. Wa kwanza usiku wa leo ni mwanamume.

234 Sasa, tuliona jana usiku, wakati mwanamke mmoja alipomjia Bwana Yesu, alienda kisimani kuchota maji, Yesu akazungumza naye kwa muda kidogo, na—na papo hapo akapata shida yake, ndipo akasema, “Nenda, kamwite mumeo.”

Akasema, “Sina mume.”

Kasema, “Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye wako.”

Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii.”

235 Sasa, wale marabi wakuu, na walimu, na watu wa kanisa walisema, “Yeye ni ibilisi.” Je, mlijua ibilisi ndiye aliyemkiri kuwa ni Mwana wa Mungu, nao wahubiri wakakiri ya kwamba Yeye alikuwa ni ibilisi? Huo ulikuwa wakati mmoja ma—mashetani walisema kweli.

236 Waangalieni Paulo na Sila wakishuka, maskini yule mpiga ramli ameketi pale, ndipo maskini mpiga ramli huyo akasema, “Hawa ni watu wa Mungu wanaotwambia njia ya Uzima.”

Wahubiri wakasema, “Wao ni makuruta, wanaupindua ulimwengu, wao ni walaghai.” Mnaona?

237 Mnaona, ibilisi huyo alijua mengi kumhusu Mungu kuliko wao walivyojua. Hiyo ni kweli. Sasa, lakini sivyo ilivyo kwa ndugu zangu siku hizi, hawa ni watu, sisemi kuhusu wahubiri hapa, hawangekuwa wameketi hapa kama waliamini hivyo, wangekuwa wameondoka. Wameketi hapa kwa sababu wanaliamini, walihubiri juu yake, waliliamini; wamesimama pembeni mwa barabara, wakalia, wakaomba. Mungu ashukuriwe tunaishi kuona siku ambazo Yeye anaitimiza ahadi Yake. Wachungaji wenu, mnapaswa kuwajivunia, ninawajivunia, nami ninajua Yeye anawajivunia, pia, watu wa Mungu.

238 Sasa, mtu huyu aliyesimama mbele yangu, simjui huyu mtu. Yeye ni mdogo sana wa umri kuliko mimi. Sijawahi kumwona maishani mwangu, nijuavyo mimi. Lakini amesimama hapa kwa kusudi fulani. Sasa, huenda ikawa ni mtu aliyeoa, akiwa na matatizo ya kinyumbani nyumbani mwake, huenda akawa ni mgonjwa, huenda ikawa amesimama kwa niaba ya mtu mwingine, labda mahitaji ya kifedha, sijui yuko hapa kwa sababu gani, sina habari, sijawahi kumwona maishani mwangu, bali amesimama hapo.

239 Sasa, vipi kama yeye ni mgonjwa? Vema, kama yeye ni mgonjwa, nisingeweza kumponya. Lakini ninii pekee. . .Kama Yesu alikuwa amesimama hapa, asingeweza kumponya. Ni wangapi wanaojua hilo? Tayari amemponya. Mnaona? Lakini jambo pekee ambalo Yesu angeweza kufanya lingekuwa ni kumjulisha kwamba Yeye angali alikuwa ni Yesu aliyetoa ahadi (Hiyo ni kweli?), aliyefanya hiyo kazi.

240 Kwa hiyo basi, kama mtu huyu akiamini, angeponywa. Kama ilikuwa ni tatizo la kifedha, angejua ya kwamba Mungu alijali kisa chake kwa sababu kilionekana mbele Zake, sio mwanadamu, bali Mungu. Mnaona? Sasa, kama Roho Mtakatifu . . . Mtu huyu aliinua mkono wake kwamba sikumjua, yeye, mimi simjui, wala yeye hanijui. Laiti Roho Mtakatifu angemfanyia jambo fulani sasa!

Sasa, kama ningeenda kule, na kusema, “Bwana, wewe ni mgonjwa?”

Angesema, “Naam, bwana, ni mgonjwa.”

“Mungu alinituma na karama ya uponyaji. Unaamini hilo?”

“Naam, bwana, ninaamini.”

Nimwekee mikono, “Nenda, upate afya katika Jina la Yesu.”

241 Ninaamini angepona. Hakika, ninaamini Mungu ana karama kote, zikifanya kazi kote kanisani kila mahali, ninanaamini hivyo. Ninaamini ya kwamba karama za uponyaji ziko kanisani. Si lazima uwe mhubiri, hata, kuwa tu mshiriki wa kawaida, mtu yeyote, ukijisikia kuongozwa kwenda kumwombea mtu fulani, nenda kafanye hivyo, hiyo ni karama ya uponyaji ikitenda kazi ndani yako.

242 Lakini sasa, yeye ange—kidogo angelitilia shaka. Lakini vipi kama Roho Mtakatifu akija na kumwambia jambo fulani ambalo amekuwa, jambo ambalo hakupaswa kufanya, ama jambo fulani alilofanya, ama jambo fulani alilopaswa kufanya, wala hakulifanya, amwambie tatizo lake, au amwambie yale yamekuwako? Kama anajua yaliyokuwako, hakika Yeye atajua yatakayokuwako basi. Hiyo si ni kweli?

243 Sasa, kama Yeye atafanya jambo kama hilo, kila mtu hapa itabidi ajue linatoka kwenye nguvu fulani. Ungeamini kuwa ni ahadi ambayo nimewasomea usiku wa leo, na kuwahubiria kutoka katika Biblia, kwamba ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu?

244 Vema. Sasa, kwa kicho kadiri uwezavyo kuwa, maana, unaona, na kila mtu awe na kicho tu, msisogee, maana ninaishika roho yako, unaona. Nami na—nataka kujua . . . Iweni tu katika maombi maaminifu.

245 Sasa, hili ni lisiloweza kukosea, kama vile Mungu asivyoweza kukosea . . . Sina njia ya kumjua mtu huyu, alishuka akaja hapa, nao wakasambaza kadi za maombi, wao walikuja hapa na kuchanganya lundo kubwa la kadi za maombi, na kuanza kuzisambaza. Hiyo inaonyesha huyo mvulana anayezitoa asingeweza kusema, “Kama ukinipa dola tano, nitakuweka mstarini.” Hawajui, kwa sababu wanachanganya kadi moja kwa moja mbele zenu, wanakupa tu yoyote unayotaka.

246 Huenda mmoja akapata namba moja, huyo mwingine apate namba kumi na tano, huyo mwingine apate tisini na tano.

Ndipo basi—basi wanapokuja, hakuna mtu anayejua mahali tutakapoanzia kuita, mpaka nitakapofika hapa. Basi popote Bwana aniongozapo, ninaita tu kuanzia hapo. Wakati mwingine huita wachache kutoka *hapa*, na wengine kutoka *hapa* nyuma, na wengine kutoka *hapa*. Ni wangapi wameona hilo likifanywa? Kuzunguka, na kuzunguka, kuzunguka kila mahali. Kwa hiyo sisi hapa tumesimama hapa, nanyi huko nje bila kadi zenu.

247 Sasa, bwana, ninataka tu kuzungumza nawe kwa dakika moja. Bila shaka umesimama hapo, moyo ukilia, "Yesu," unainua mkono wako, bila shaka ungenipa kujua ya kwamba wewe ni Mkristo, ama ungeweza tu kuwa unaiga jambo hilo, unaona, ukitenda tu kama ndivyo ulivyokuwa. Kama ndivyo, kama ndivyo alivyo, angalia kinachotukia. Sasa, wameingia kisiri mstarini mara nyingi, wamewabeba wakawatoa nje, na kadhalika.

248 Kwa hiyo, kama Bwana Mungu ataniambia jambo fulani kuwahusu, kusanyiko hili linalongojea, jambo lililokuleta hapa, sababu yako ya kusimama hapa jukwaani, ungeweza kuwa mwamuzi kama ilikuwa ni kweli ama si kweli. Je, ungefanya hivyo? Ungejua kama ilikuwa ni kweli. Na kama ni kweli, utakuwa tayari kusema ni kweli; kama ni uongo, useme ni uongo, hivyo tu.

249 Umekuja nikuombee, kwa ajili ya ugonjwa mwilini mwako, na ugonjwa huo ni kivimbe ubavuni mwako. Um-hum. Unaamini? Sasa, sasa, anaonekana kuwa na mawasiliano mazuri na Mungu sasa hivi, linalomwezesha mkosoaji, ama kitu fulani, ambaye labda amesimama karibu, apate kujua kwamba kamwe hakubahatisha.

250 Sasa, sasa hivi, sijui nilichomwambia. Njia pekee nijuayo ni hiki kinasa sauti kilichowekwa hapa, ndipo kanda itakaporudi, kesho yake watanichezea; ni kama ndoto. Sasa, huyo hakuwa ni mimi. Sijui lolote kumhusu mtu huyo, mnaona, si zaidi ya vile maikrofoni hii inavyojua kuzungumza, haina budi kuwa na kitu kilicho hai kikinena ndani yake. Simjui huyo mtu, kwa hiyo haina budi kuwa ni Mungu anayenena mle ndani.

Sasa, nachukua tu wakati wangu, kama nikimweka tu mmoja hapa kwa muda kidogo, ili kwamba tu mpate kujua, mnaona, hilo linapaswa kuwaridhisha wote.

251 Sasa, hebu kidogo tu, bwana, ninataka tu kuwasiliana na roho yako. Hilo ndilo jambo lile lile alilofanya Bwana wetu alipozungumza na yule mwanamke kisimani, kasema, "Nipe maji ninywe," mnaona. Alikuwa tu akijaribu kushi-. . .Baba alimtuma huko juu.

252 Alikuwa na haja kupitia Samaria, lakini alipofika kule, huyo mwanamke akatokea, kwa hiyo ilimbidi Yeye kuzungumza naye, kuwasiliana na roho yake, hilo ndilo jambo lile lile ninalofanya sasa hivi. Naam, ninakiona, ni kivimbe katika ubavu wako wa

kulia, una kimoja mkononi mwako, pia. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Ni watu watatu tu ulimwenguni waliojua habari zake, hao walikuwa ni yeye na dada yake, bali kuna Mmoja juu aliyejua habari zake.

253 Sasa, hebu tuzungumze naye kwa dakika moja. Umekuwa ukimwombea mtu mwingine, pia, mtoto, ugonjwa wa findo, uliyeketi moja kwa moja hapo nje. Atakuwa mzima, kwa hiyo usimhofie tena.

Unaamini?

Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Bw. Morrison, Jack, nenda nyumbani, uwe mzima.

"Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana kwao waaminio."

254 Sasa, kama sikukwambia neno moja, na nikuombee tu, unaamini kuna upako hapa jukwaani? Unaamini? Ungeamini hilo? Vipi kama ningekwambia, uliponywa kabla ya kuja kule, ungeamini? Vema, unafikiri nini juu ya mjukuu wako? Unafikiri angepona, pia? Vema. Nenda zako na uamini. Mwekelee leso hiyo.

Unaamini? Amini.

255 Wewe ni mtoto tu kwangu, msichana. Sikujui, lakini hii hapa picha ile ile kama katika Yohana Mtakatifu mlango wa 4, mwanamke na mwanamume. Msichana wa kupendeza anasimama hapa, anaonekana mwenye afya awezavyo kuwa. Sijui lolote kumhusu, sijawahi kumwona maishani mwangu. Hatufahamiani, sivyo, mama? Naam, bwana, hatufahamiani.

256 Ikiwa Mungu ni Neno la Mungu, ambalo ni Kristo aliyefanyika mwili, na kama anaweza kufanyika halisi miilini mwetu, ambayo aliitakasa kwa Damu Yake Mwenyewe, akimtuma Roho Wake Mtakatifu afanye maskani. . .Mungu alikuwa ndani ya Kristo. Mungu alishuka na kujijengea, akapiga hema, kama mwanadamu. Yeye—Yeye alibadilisha sura Yake na akawa mwanadamu, Mungu alifanya hivyo, apate kulitakasa Kanisa ambalo angeweza kuishi ndani yake, na kwa miaka elfu mbili akafanya miujiza Yake, na kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu yeye yule akiishi ndani ya watu Wake, Mungu akifanya maskani ndani ya mwanadamu.

257 Kama Mungu atanifunulia, kwa Roho Wake, shida yako ni nini, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Unaamini hilo? Je, ungekubali kuwa limetoka kwa Mungu? Basi utamkumbatia mtoto huyo mchanga unayemtaka, unayemwombea. Nenda zako, amini, ninakupa mtoto huyo katika Jina la Yesu Kristo. Nenda, ukampokee. Usiwe na shaka. Ulimtaka huyo kwa muda fulani. Vema. Nenda, ukiamini.

"Kama unaweza kuamini." Unaamini?

258 Vema, mama, sikujui. Hebu kidogo, wewe ni. . .Inaanzia jengoni sasa, Hiyo hapo imetoka, na kuondoka jukwaani, ikaingia jengoni. Mtu fulani alimgusa, hakika kama ninavyosimama hapa.

259 Yupo msichana aliyesimama hapa, siwezi kuona alipo. Ninamwona, ana ugonjwa wa shingo, yabisi kavu ya uti wa mgongo. Kama utaamini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo anakuponya. Likubali, amini, maskini mama huyo aliyeketi hapa amevaa miwani, nywele nyeusi, simama. Ninakupa uponyaji wako, katika Jina la Yesu Kristo.

260 Aligusa nini? Mwulizeni huyo mama. Sikujui, sivyo, mama? Sikujui, sivyo? La. Kama sikujui, inua mkono wako, utikise mkono wako. Kama hiyo ilikuwa ndiyo shida yako, yale Yeye aliyokwambia, tikisa mkono wako. Sasa umeponywa.

261 Aligusa nini? Yuko futi thelathini kutoka kwangu. Alimgusa Kuhani Mkuu, Naye akatenda tu kama alivyotenda hapo mwanzo. Sasa, huyo ni Yesu yeye yule, yeye yule jana, leo, na hata milele. Amini, usiwe na shaka.

262 Baadhi yenu wengine, naipa changamoto imani yenu kuamini, sio mimi, aminini Neno la Mungu, aminini niliwaambia kweli. Ninatoa changamoto kwa imani yenu ku—kuamini hilo.

263 Papo hapo nyuma yake, ulifanya hivyo, sivyo, mama? Unayeketi papo hapo nyuma yake hapo, umeketi hapo ukiwa na shinikizo kuu la damu, simama kwa miguu yako. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Kama sikujui, inua mkono wako mwingine. Ninakupa uponyaji wako, katika Jina la Yesu Kristo. Ulimgusa, Yeye hakika anajua kukuhusu. Nenda zako nyumbani, na uwe mzima.

Mwaminini Mungu, msiwe na shaka. Unaamini kwa moyo wako wote?

264 Kitu cha kigeni kumhusu, sikujui, Mungu anakujua. Uh-huh. Unaamini Mungu atakuponya, na kukupa afya? Wewe hutoki hapa, unatoka mahali panapoitwa Huntington. Jina lako ni Bibi Day. Unamwombea ndugu fulani, ndugu mmoja yuko Galveston hospitalini, yeye ni m—mraibu. Nenda, amini, usiwe na shaka, Yesu Kristo anakuweka huru, katika Jina la Yesu Kristo.

Mwamini Mungu. Unaamini?

265 Vipi kama sikukwambia lolote, nikakuwekea tu mikono, ungeamini, mama? Njoo hapa. Pokea uponyaji wako, katika Jina la Yesu Kristo. Nenda, amini.

Vipi kama nilikwambia hicho kisukari kingekwisha, ungeamini? Nenda, amini, usiwe na shaka.

266 Ulipokuwa umeketi papa hapa chini muda mfupi uliopita, unaona, nilikuona ukiugua ugonjwa wa moyo. Pia una kasoro

mgongoni mwako. Sasa nenda ukiamini, nawe utapata afya kama ukiamini kwa moyo wako wote.

267 Njoo, msichana. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Wewe ni msichana mdogo, lakini una shida ya kike, kudondoka, ni ovari yenye usaha. Usiwe na shaka, amini. Nenda, na kamwe halitatukia tena, unaweza kuwa mzima. Amini kwa moyo wako wote.

268 Unaamini kwa moyo wako wote? Unaona, kama utaamini tu sasa, ni Roho Mtakatifu akitenda kazi kikamilifu.

Vipi kama ningekuwekea tu mikono, ungefikiri ungepona? Njoo, mama.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

269 Njoo, ukiamini. Kama sikusema neno moja kwako, ungeamini kama nikikuwekea mikono, ungepona? Vema, njoo, na hicho kisuka-. . . Vema, endelea, kisukari kitakuwa sawa, utapona. Nenda, amini kwa moyo wako wote.

270 Unaamini kwa moyo wako wote, kila mtu? Aminini sasa. Sasa angalia tu, sasa, Yeye alisema nini? Mnajua kuna namna fulani ya upako hapa mahali fulani unaowajua. Mnaamini hilo?

271 Maskini mama mmoja aliyeketi hapo akiomba, akitikisa kichwa chake huku ana ugonjwa wa moyo, koma, acha, acha kuogopa, amini kwa moyo wako wote, utapona, kwa vyovyote vile. Mungu atakuponya.

272 Huyo mama aliyeketi hapo nje akimwombea mwanawe ambaye hajaokoka, amini kwa moyo wako wote, Mungu atamshughulikia kwa ajili yako. Sikujui, sivyo, mama? Sikujui hata kidogo, bali hilo ndilo ulilokuwa ukiombea. Nilijuaje ulichokuwa ukiombea? Mungu anayesikia maombi anaweza kujibu maombi. Amina.

Unaamini kwa moyo wako wote? Kuwa na imani. Sasa iweni na kicho.

Njoo, hebu nikuwekee mikono sasa, wakati upako wa Roho Mtakatifu ukiwa hapa.

Katika Jina la Bwana Yesu, jalia aponywe. Amina.

Nenda, ukiamini.

273 Unajua, kwa kweli, wasiwasi wako ndio uliosababisha jambo hilo, ulifanya tumbo lako namna hiyo. Sasa, amkeni tu usiku wa leo, na kusema, "Nimemalizana nao, ninamwamini Mungu," kisha uende ukale chakula chako cha jioni, utakuwa sawa, nenda ukaamini kwa moyo wako wote. Katika Jina la Bwana Yesu.

274 Huenda mtu fulani akasema, "Wewe, kama wewe ni mzee, moyo wako ni dhaifu, kwa vyovyote vile." Lakini sivyo, una moyo wenye wasiwasi, umekuwa nao kwa muda mrefu. Nenda, amini

kwa moyo wako wote, utapona, nawe utaenda nyumbani, uwe mzima. Amini kwa moyo wako wote.

275 Unampenda Bwana? Jambo fulani limetukia, lakini siwezi kulipata, ni ninii tu, kila kitu kinaingia ukungu kwangu sasa. Mnaona? Ni wangapi wanaojua ya kwamba maono yanafanya hivyo? Danieli aliona moja, akafadhaika kichwani mwake kwa siku nyingi. Ni wangapi wanaojua hilo? Mnaona? Hakika. Mwanamke mmoja aligusa upindo wa vazi la Bwana, Naye akasema, "Nguvu zimenitoka."

Vema, Dada, njoo ukiamini sasa, kamwe hautakulemaza.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Utukufu!

Amini kwa moyo wako wote.

276 Unaamini kwa moyo wako wote, kila mtu? Ni kitu gani kingeweza kutukia sasa hivi? Lolote lingeweza kutukia. Hakika, unajua ya kwamba *Kitu fulani* kipo hapa. Mungu unayemtumikia yu pamoja nawe sasa.

277 Ninamwona mama mmoja ameketi hapa ameinua kichwa chake, anaomba, Nuru hiyo inaning'inia moja kwa moja juu yake. Ninahofia tu hatalipata. Ana ugonjwa wa utumbo na mgongo. Ee Mungu, natumaini yeye. . .Bibi Dickman, simama na ukubali uponyaji wako. Vema. Mungu akubariki, huyu mama hapa aliyevaa sweta nyekundu ndiye.

278 Papa hapa mwishoni mwa safu, kuna mwanamume na mwanamke walioketi hapo, huyo mwanamke amekuwa na matatizo mengi. Amefanyiwa upasuaji karibu dazani moja, ana shida ya ini, mumewe ana ugonjwa wa ateri. Bw. na Bibi Main, aminini kwa moyo wenu wote, na mwende nyumbani mkaponywe. Yesu Kristo anawaponya.

Ninawapa changamoto mtazame huku na kuliamini. Ninawaomba mliamini. Haleluya! Ni wangapi wanaoamini kwa moyo wenu wote?

279 Loo, rafiki mwenye dhambi, ungetaka kumpokea huyu Yesu? Ninyi mlioinua mikono yenu mlikuwa wenye dhambi, njoni hapa kwa dakika moja, hebu niwawekee mikono, hivi mtakuja? Njoo papa hapa chini sasa, rafiki mwenye dhambi. Njoo hapa, ninakualika kwa Kristo. Njoo, hebu nikuwekee mikono. Kama Mungu anaujua moyo wako, anataka usamehewe dhambi zako.

280 Njoo sasa hivi, hapa madhabahuni, hivi utakuja? Kila mwenye dhambi humu jengoni anayetaka kumpokea Yesu kama Mwokozi wao, shuka moja kwa moja sasa, kila mmoja, kweli, wakati Roho Mtakatifu anapotia mafuta. Shuka moja kwa moja chini, hiyo ni kweli.

281 Njoo kila mtu aliyekandamizwa na dhambi, kuna rehema kwa Bwana. Hivi hutakuja? Njoni moja kwa moja huku. Hilo ni sawa tu. Njoni, kila mwenye dhambi asiyemjua Mungu, unataka

kukumbukwa sasa katika maombi, na unataka Mungu aiokoe nafsi yako, wakati akiwa hapa.

282 Roho Mtakatifu alinisimamisha wakati uo huo, akasema, "Ita! Nina watoto wanaongojea huko nje." Mungu yeye yule anayeweza kuzungumza bila kukosea, hivi hawezi kusema jambo lile lile? Sasa ndio wakati, sasa ndio wakati. Tokeni, kila mtu anayetaka kumchukua Kristo kama Mwokozi, njoni madhabahuni hapa kwa muda kidogo tu. Mtafanya hivyo?

> Njoo, kila nafsi iliyokandamizwa na dhambi,
> Kuna rehema kwa Bwana,
> Naye hakika atakupa raha,
> Kwa kulitumainia Neno Lake.
>
> Mtumaini Yeye tu . . .

283 Anakujua. Njoo sasa, hivi utakuja? Njoo umtumaini. Hivi unataka kuwa kama maskini yule mama kulungu? Unataka tukio halisi na Mungu? Njoo kwa mmoja, njoo kwake Bwana Yesu, Yule awezaye kukupa tukio hilo. Mshiriki wa kanisa, hivi umefadhaika? Njoo sasa. Njoo, ewe mshiriki wa kanisa.

> . . . wewe,
> Atakuokoa sasa.

284 Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, Mlutheri, Mkatoliki, Mpentekoste, ambaye huna hakika na ujuzi wako, utakuja? Hatukuombi ujiunge na kanisa lolote. Tunakuomba tu uje hapa na kusimama kwa ajili ya maombi. Ulitaka kuona kitu halisi. Ni kitu gani kilicho halisi zaidi ya Yesu Kristo aliyefufuka katika wafu katika kizazi kiovu na cha zinaa, akijionyesha Mwenyewe ya kwamba amefufuka katika wafu, kama Yona, aliyetoka katika tumbo la nyangumi? Yeye yu hai milele. Hivi hutakuja sasa, tunapouimba tena?

> Mtumaini Yeye tu . . . ( . . . ? . . . )
> . . . Yeye atakuokoa,
> Loo, Yeye ataokoa . . . (Njoo ndugu yangu Mpresbiteri . . . ? . . . )
>
> Mtumaini Yeye tu . . .

285 Kila mwanamume ama mwanamke ambaye hana Roho Mtakatifu, hebu na wasimame kwa miguu yao sasa, wote wanaomtaka Roho Mtakatifu.

> Loo, Yeye atakuokoa, atakuokoa,
> Atakuokoa sasa.

286 Ninataka kuwaomba ndugu wahudumu hapa jukwaani kama wanaweza, na wanaweza kuwazunguka hawa wenye dhambi waliotubu hapa, ninawatakeni mshuke mje, tunataka kuwawekea mikono, tuombe pamoja nao, tuwatoe nje, muwaalike makanisani mwenu, popote walipo, na wawe washiriki.

287 Angalieni, enyi marafiki, ninyi mliosimama hapa, kuna jambo moja tu. . . Hebu niwaonyeshe kile kilichotukia. Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu." Basi Mungu alikuleta hapa, kamwe hakukuleta hapa bure. Ulisimama kutoka kwenye kiti chako na ukaja, hivyo tu ndivyo unavyoweza kufanya ili kuungama. "Yeye atakayenikiri Mimi mbele za watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu." Hivyo ndivyo alivyoahidi. "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi, hatakufa kamwe."

288 Ninawauliza sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa ajili ya maombi, ni wangapi hapa ndani sasa ambao ni wagonjwa na wanateseka bado? Inueni mikono yenu. Sasa, wekeaneni mikono. Weka ninii yako . . .

61-0119E Malkia Wa Sheba
American Legion Hall
Beaumont, Texas Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org